



Kujitayarisha na Kushughulikia Visa vya Unyanyasaji wa Kijinsia Wakati wa Dharura

MWONGOZO WA UJUMUISHAJI WA WANAWAKE NA WASICHANA ANUWAI



Zawadi ya Serikali ya Marekani

Iliandaliwa 2019

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura
Mwongozo wa ujumuishaji

Shukrani

Shirika la Kimataifa la Uokoaji (IRC) lingependa kuwashukuru wanawake na wasichana anuwai, watetezi wa haki za wanawake, mashirika, mitandao na wahudumu wanaoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia (GBV) ambao wamechangia utayarishaji wa mwongozo huu.

Shirika la IRC lingependa kushukuru sana hasa washiriki wa **Mpango wa Building Local Thinking Global (BLTG)** kwa kuendelea kutoa msaada kwa watendaji wanaotumia mwongozo huu: [Akina Mama wa Africa](#), [GBV Prevention Network](#), [Women's International Peace Centre](#), [El-Karama](#), [Gender Equality Network – Myanmar](#), na [Strategic Initiative for Women in the Horn of Africa](#).

Kwa pamoja wanachama wa mpango wa BLTG wanashirikiana katika mpango wa kimataifa, unaohusisha mashirika mmbalimbali ambao unalenga kukuza uongozi wa wanawake wenye mabadiliko katika kujiandaa na kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia katika miktadha ya dharura. Sisi ni watetezi wa usawa wa wanawake, haki za wanawake, mashirika ya mashinani, wanaharakati, wasomi, mashirika ya kitaifa, kikanda na ya mtandao, yanayofanya kazi katika miktadha ya dharura na maeneo hatari na tumejitolea katika ulinzi na uwezesaji wa wanawake na wasichana. Unaweza kupata habari zaidi kuhusu BLTG [hapa](#).

Shirika la IRC linatambua kwa shukrani kazi ya msingi ya Inbal Sansani, Jennate Eoomkham, Sarah Cornish-Spencer na Ricardo Pla Cordero.

Shirika la IRC linashukuru [Ofisi ya Kuhesabu Watu, Wakimbizi, na Uhamiaji - Idara ya Majimbo ya Marekani](#) ambao wamefadhili mradi wa BLTG tangu 2017 kama zawadi ya Serikali ya Marekani.

YALIYOMO

UTANGULIZI	4
Usuli	4
Kwa nini kujumuishwa kwa wanawake na wasichana anuwai katika kuandaa mpango wa kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia katika miktadha ya dharura ni muhimu?	5
Ni nani anafaa kutumia mwongozo huu?	5
ISTILAHU NA UFAFANUZI	7
Vidokezo vya istilahi za kutumia na za kuepuka	9
HATARI NA VIKWAZO VINAVYOWAKABILI WANAWAKE NA WASICHANA ANUWAI	10
Wasichana waliobalehe	14
Wanawake waliokomaa zaidi	16
Wanawake na wasichana wenye ulemavu	19
Wanawake na wasichana wenye mwelekeo tofauti wa kingono na utambulisho tofauti wa kijinsia	21
Wanawake na wasichana wanaohusishwa na kabila au dini tofauti	24
HATUA MUHIMU KATIKA KUBUNI MIPANGO JUMUISHI YA KUSHUGHULIKIA UNYANYASAJI WA KIJINSIA	28
Tathmini	28
Jinsi Mpango Ulivyoandaliwa	32
Kushughulikia Visa vya Unyanyasaji wa Kijinsia	33
Msaada wa Kisaikolojia	38
Nafasi salama za Wanawake na Wasichana (WGSS)	40
Huduma za Afya	42
Mifumo ya Uelekezaji	44
Kufikisha Huduma kwa Jamii	45
Kupunguza Hatari kwa Wanawake na Wasichana katika Miktadha ya Dharura	46
Kudhibiti na Kushiriki Habari	48
Uratibu na Utetezi	50
Kuwa Tayari na Mipango ya Kukabiliana na Dharura	52

UTANGULIZI

Mwongozo huu unaambatana na [kielelezo, zana za kutathmini](#) na [nyenzo za mafunzo](#) za shirika la IRC za kujitayarisha na kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia katika miktadha ya dharura [haufai](#) kutumiwa peke yake kushughulikia masuala ya uanuwai na ujumuishaji. Mbinu zinazotumiwa peke yake za kukabiliana na uanuwai na utangamano wa vigezo zinaweza kosa kufanikiwa katika kujumuisha hatua shirikishi kwenye shughuli za kila siku za kutoa misaada ya kibinadamu. Hivyo, maudhui ya mwongozo huu yatakaposasishwa tena yatajumuishwa katika kifurushi cha mafunzo ya kujitayarisha na kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia katika miktadha ya dharura. Kwa sasa, mwongozo huu unashughulikia pengo katika kujumuisha kimaksudi wanawake na wasichana anuwai katika kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia. Mwongozo huu unaweza kutumika kama sehemu ya kielelezo cha kushughulikia visa hivi vya unyanyasaji katika miktadha ya dharura ili kusaidia wanaoshughulikia visa hivyo kuchunguza mitazamo, ujuzi na maarifa yao wenyewe na kuchukua hatua thabiti za kufikia na kusaidia wanawake na wasichana anuwai katika mipango ya kujitayarisha na kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia katika miktadha ya dharura.

Usuli

Wanawake na wasichana wanahusika pakubwa katika ulinzi wao. Ni muhimu washiriki kamilifu katika mchakato wa kutambua hatari za ulinzi na suluhisho katika mipango ya kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia katika miktadha ya dharura. Mradi wa [Building Local Thinking Global Initiative](#) unasaidia watoa huduma wanaoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia katika maeneo husika kuhakikisha kuwa uwezo wa wanawake na wasichana kufikia na kushiriki kutoka mwanzo wa matukio ya dharura unaleta matokeo bora zaidi katika mpango wa kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia. Mwongozo huu unalenga kushughulikia hatari na vizuizi vingi vya upatikanaji wa huduma vinavyowakabili wanawake na wasichana kutoka maeneo mbalimbali. Lengo letu ni kwamba wanawake na wasichana wote waweze kupata huduma kwa njia salama na waweze kushiriki kikamilifu katika mipango jumuishi ya kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia.

Wanaoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia wanapotatua vizuizi na ubaguzi ambao unawakabili wanawake na wasichana anuwai katika miktadha ya kibinadamu, hatua hii inahakikisha kuwa wanawake na wasichana **WOTE** wananufaika kutokana na mpango wetu na wanalindwa dhidi ya hatari na kusaidiwa ili wapate nafuu na wajiendeleze.¹ Kutokana na maombi kutoka kwa watoa huduma wa maeneo husika katika mradi wa Building Local Thinking Global, mwongozo huu umezingatia vigezo vifuatavyo vya ukosefu wa usawa vinavyotangamana na vinavyoathiri wanawake na wasichana anuwai: ubaguzi kwa misingi ya umri kwa walio wazee zaidi, ujana, ulemavu, mwelekeo wa kijinsia, utambulisho wa kijinsia, kabila, mbari au dini ambayo mtu anahusishwa nayo. Kwa hivyo, mwongozo huu haujashughulikia masuala yote na katika kila eneo, kutakuwa na wanawake na wasichana wanaokabiliwa na ubaguzi wa kiwango cha juu kutokana na vigezo vya ukosefu wa usawa vinavyotangamana ambavyo havijashughulikiwa kikamilifu katika mwongozo huu. Wanawake na wasichana hawa ni pamoja wale walio na VVU, wanaohusika katika biashara ya ngono, wahamiaji na wale wasio na uraia wa nchi yoyote. Ingawa haujagusia masuala yote, mwongozo huu unajumuisha kanuni na mbinu ambazo zinaweza kutumiwa kwa busara kurekebisha mipango inayoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia ili ifikie wanawake na wasichana anuwai katika miktadha tofauti ya kibinadamu. Miongozo ya ziada ya wadau mbalimbali inaweza kupatikana katika sehemu mbalimbali za mwongozo huu ili kuwapa wanaohudumia visa vya unyanyasaji wa kijinsia nafasi za kujifunza kuhusu mada fulani.

¹ GBV Emergency Response Model Outcome <https://gbvresponders.org/emergency-response-preparedness/emergency-response/>

“Utangamano wa vigezo unahusu jinsi tunavyochukulia utambulisho na vile unavyohusiana na nguvu”

Kimberlé Crenshaw, Mapping the Margins: Intersectionality, Identity Politics, and Violence Against Women of Color (1994) <https://www.racialequitytools.org/resourcefiles/mapping-margins.pdf>

Kwa nini kujumuishwa kwa wanawake na wasichana anuwai katika mpango wa kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia katika miktadha ya dharura ni muhimu?

Kila muktadha wa kibinadamu una wanawake na wasichana anuwai. **Wanaohudumia visa vya unyanyasaji wa kijinsia wanapaswa kujaribu kuwaelewa wanawake na wasichana katika uanuwai wao, na kuchukua hatua kuhakikisha kuwa mipango ya kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia inajumuisha na kushughulikia mahitaji, vizuizi na hatari ambazo wanawake na wasichana anuwai wanakabiliana nazo.** Wanawake na wasichana anuwai wanakabiliwa na aina nyingi za ukandamizaji ambazo hupunguza zaidi nguvu zao, chaguo na ulinzi dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia, na kuongeza vizuizi vinavyowazuia kupata huduma. Wanawake wengine waliohamishwa na wale wenyeji pia watawezesha na kulindwa na hali yao ya kijamii. Wale wanaoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia wanafaa kuhakikisha kuwa hawahudumii wanawake wazima walio na nafasi katika jamii ambao wametoka katika madaraja ya juu au hali ya juu ya kiuchumi na kijamii pekee, yaani wamesoma, wana mahusiano na jinsia tofauti, ni wazima kimwili, wanaojitambua na jinsia waliozaliwa nayo, au hawana VVU; au wanahusishwa na kabila au dini kuu.

Kanuni elekezi za unyanyasaji wa kijinsia, pamoja na maadili na kanuni pana zinazoongoza utoaji misaada ya kibinadamu, zinahitaji hatua mahususi ili kuendeleza ujumuishaji wa **wanawake** na wasichana katika mipango ya kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia. Kanuni ya kibinadamu ya **kutopendelea** - kutoa msaada kwa misingi ya haja na bila ubaguzi - inahitaji wafadhili na mashirika ya msaada kupunguza vizuizi ili watu **wote** katika jamii husika waweze kupata msaada kwa misingi sawa na yenye usawa na watu wengine.² Katika Kanuni za vuguvugu la Sphere, kugawanywa kulingana na jinsia, umri na ulemavu ni kigezo msingi katika kushughulikia mahitaji ya watu walio hatarini.³ **Kutengwa** kwa wanawake na wasichana anuwai katika kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia katika miktadha ya dharura huongeza viwango vya waathiriwa, athari za kisaikolojia na matatizo ya kiafya. **Ubaguzi** huu ni aina ya dhuluma ambayo hupunguza uwezo wa wanawake na wasichana kukidhi mahitaji yao ya kimsingi na huwaongezea hatari ya kudhulumwa zaidi. **Ujumuishaji hauhitaji** ujuzi wa kitaalam bali unahusu **kushughulikia vizuizi** vinavyozuia uhakikishaji usalama na uwezeshaji sawa wa wanawake na wasichana katika hatua zinazochukuliwa kwenye miktadha ya kibinadamu.

KUMBUKA! Katika kila muktadha, ni wanawake na wasichana walio katika hatari kubwa ya kuathiriwa na unyanyasaji wa kijinsia. Hii inatokana na nafasi yao ya chini katika ngazi ya jinsia, ukosefu wa usawa unaotokana na sababu hii, na nguvu na upendeleo wanaopata wanaume na wavulana ulimwenguni.

Ni nani anafaa kutumia mwongozo huu?

Wahudumu wanaoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia wanaotumia [kielelezo](#), [zana za kutathmini](#) na [nyenzo za mafunzo](#) za shirika la IRC za kujitayarisha na kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia katika miktadha ya dharura, wanaweza kutumia dokezo hili la mwongozo ili kuhakikisha kuwa wanawake na wasichana anuwai wanapata usaidizi kupitia mpango wa kujitayarisha na kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia katika

² ADCAP Training, p. 22. <https://www.helpage.org/what-we-do/emergencies/adcap-age-and-disability-capacity-building-programme/>

³ Sphere Standards. <https://www.spherestandards.org/handbook-2018/>

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura
Mwongozo wa ujumuishaji

miktadha ya dharura. **Mwongozo huu unawalenga wahudumu na wakala maalum ambao tayari wamepata mafunzo na wana ujuzi katika kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia.** Mwongozo huu uliandaliwa kupitia na unapaswa kutumiwa kimsingi na wanachama wa mradi wa Building Local Thinking Global, ili kusaidia watoa huduma wanaoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia na mashirika ya haki za wanawake kutumia mipango jumuishi ya kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia wakati mzozo wa kibinadamu unaathiri watu fulani.

Dokezo hili la mwongozo na mwongozo wa mafunzo unaotumiwa pamoja zimebuniwa kusaidia wanaoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia kutafakari, kujifunza na kuchukua hatua za kutekeleza mipango jumuishi ya kushughulikia visa hivi vya unyanyasaji kwa ajili ya wanawake na wasichana anuwai. Wakati wa kutumia mwongozo huu, tunakuhimiza:

- **Utambue kuwa suala hili linatuhusu sisi na ujiepushe na kuwaona wengine:** Wanawake wafanyikazi na wanaojitolea wanaoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia huwa wamekumbana na ubaguzi kwa sababu ya jinsia yao, mbari, daraja, ulemavu, mwelekeo wa kingono, utambulisho wa kijinsia, kabila au dini. Epuka kuelezea ujumuishaji kana kwamba utambulisho na matukio haya yanahusu wanawake **wengine** tu. Kuhusisha masuala haya na wengine ni aina ya ubaguzi na utengaji. Badala yake, toa fursa kwa wanawake kushiriki maarifa yao na yale waliyoyapitia binafsi yanayohusu upendeleo, ubaguzi na uanuwai.
- **Ujiitambue:** Kuwa makini na mitazamo na upendeleo wako. Tafakari juu ya matukio tangamano ambapo wewe mwenyewe umekumbana na ukandamizaji na upendeleo. Jua mipaka yako na uombe usaidizi ili ujifunze zaidi kuhusu vizuizi na hatari wanazopitia wanawake na wasichana anuwai. Kaa ukiwa tayari kujifunza zaidi kuhusu wanayopitia wanawake na wasichana anuwai kwani mahitaji ya wanawake na wasichana anuwai na utambulisho wa kijinsia unaendelea kubadilika.
- **Ulenge vizuizi vinavyotokana na watu na mazingira au mifumo:** Chunguza jinsi wanawake na wasichana anuwai hukabiliwa na ubaguzi na ukosefu wa usawa wa kimfumo. Haya yote huwaongezea hatari ya kuathiriwa na unyanyasaji wa kijinsia na vizuizi vinavyowakabili katika kupata huduma za kushughulikia unyanyasaji huu.
- **Usherehekee uanuwai:** Ujumbe muhimu katika mwongozo huu ni kuchukua mtazamo unaozingatia uthabiti wa uanuwai wa wanawake na wasichana, kama tunavyofanya na mipango yote ya kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia. Njia hii inatambua mambo mbalimbali wanayopitia wanawake na wasichana, na kutambua mshikamano na msaada wa pamoja ambao wanawake na wasichana wanapata katika vikundi vilivyoanzishwa kulingana na utambulisho wao anuwai. Njia hii inaozingatia uthabiti huendeleza manufaa ya kuanzisha mipango ya kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia ambayo inajumuisha wanawake na wasichana.
- **Ujitolee kujifunza:** Wahudumu wanaoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia bado wanajifunza jinsi aina tofauti za ukosefu wa usawa na ubaguzi zinaathiri wanawake na wasichana, na kufuta upendeleo na kasumba walizokuwa wamejifunza na kushikilia. Tunakuhimiza uwe tayari kujifunza na kusikiliza kila mmoja na ujitolee kuzingatia maadili ya kitaalam yanayounga mkono haki za wanawake na wasichana wote kupata huduma kwa njia salama, kuondoa vizuizi na kufanya kazi kwa pamoja kumaliza ubaguzi dhidi ya wanawake na wasichana wote. Tunashirikiana na wataalam wa eneo husika wa masuala ya wazee, ulemavu, LGBTQ, kabila na dini katika masomo yetu. Ungana na vuguvugu na wahudumu wengine wanaotetea haki za kijamii ili ujifunze zaidi.

ISTILAHU NA UFAFANUZI

- **Kuweza kufikiwa:** wakati huduma za kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia zinapatikana, zinaweza kufikiwa na kutumiwa kwa njia salama kwa wakati unaofaa na wanawake na wasichana anuwai kulingana na mahitaji yao. Katika Mtakaba wa Haki za Watu wenye Ulemavu, ufikivu umefafanuliwa kama " hatua zinazofaa za kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata (huduma) kwa njia sawa na wengine."
- **Upendeleo:** Ubaguzi dhidi ya kitu au mtu. Mara nyingi upendeleo hutokana na kasumba na husababisha mitazamo inayodhuru na mazoea ya kibaguzi, iwe au isiwe ya moja kwa moja. Watu wengi wanaweza kuwa hawajui kwamba wana upendeleo unaotokana na kaida zinazodumu za kijamii zinazobagua vikundi fulani vya watu.
- **Kujitambulisha kwa jinsia ya kuzaliwa:** Mwanamke au msichana anayejitambulisha kwa jinsia ya kike kama alivyozaliwa.
- **Ubaguzi:** **Ubaguzi wa moja kwa moja** hutokea wakati, katika hali sawa, watu fulani wanahudumiwa kwa njia duni ikilinganishwa na watu wengine kutokana na hadhi tofauti ya kibinafsi kwa sababu inayohusiana na mambo yaliyokatazwa. **Ubaguzi usio wa moja kwa moja** unamaanisha kuwa sheria, sera au desturi huonekana kutobagua yeyote lakini zina athari hasi kwa watu fulani.
- **Uwezeshaji:** Uwezeshaji ni mchakato ambapo wanawake na wasichana waliobalehe wana udhibiti zaidi juu ya maisha na miili yao: kutambua ajenda zao wenyewe, kupata ujuzi, kutatua shida na kuweza kujitegemea. Uwezeshaji huwawezesha wanawake kuchangia katika sera, michakato na taasisi zinazoathiri maisha yao, ikiwa pamoja na miundo na taasisi ambazo zinaendeleza na kukuza dhuluma, ubaguzi na ukosefu wa usawa wa kijinsia. Dhana hii ina historia ndefu katika kazi ya mabadiliko ya kijamii⁴ ambayo inasisitiza umuhimu wa kupata uwezo wa kufanya maamuzi yenye maana.⁵
- **Kutengwa:** Kutengwa kunaweza kuwa matokeo ya ubaguzi na dhuluma katika maisha ya wanawake na wasichana. Inawezekana kuwa kuna njia tunazotambua au ambazo hatutambui ambapo tunavipa vikundi vilivyotengwa nafasi za chini na kuvifanywa vijihisi kana kwamba si muhimu sana vikilinganishwa na wale wenye nguvu au fursa zaidi katika jamii.
- **Mitazamo wa kawaida wa jinsia:** Mitazamo, tabia na mifumo kulingana na dhana kwamba kila mtu anavutiwa na watu wa jinsia tofauti.
- **Utambulisho** unajumuisha vigezo tofauti vya uzoefu wa mtu na unarejelea sifa (mfano, umri, daraja, kabila, n.k) na majukumu (kwa mfano mama, mwanariadha, mwanafunzi na kiongozi) yanayounganisha watu kwa vikundi maalum katika jamii na kumpa kila mtu upekee wake. Utambulisho wa mtu huathiri jinsi anavyotazama ulimwengu, anavyoamua kutenda na yale wengine wanayomtendea. Sehemu zingine za utambulisho (mfano rangi ya ngozi) zinaonekana hadharani na zingine (mfano mwelekeo wa kingono) mtu anaweza kosa ujasiri wa kuyashiriki kutokana na unyanyapaa, hofu ya kukataliwa au kuhukumiwa.⁶ Ni muhimu kutambua kwamba utambulisho umechaguliwa na kulazimishwa. Kwa mfano, wanawake na wasichana wenye

⁴ Cornwall, p. 1. Women's empowerment: what works and why? World Institute for Development Economics Research (2014).

⁵ PAL, p. 4.

⁶ Raising Voices. Get Moving!, p. 47.

ulemavu wanaweza kutojiona kama wenye ulemavu na inaumiza kuona ulemavu kama sehemu muhimu ya utambulisho wa mtu wakati yeye haishi kwa njia hii.

- **Ujumuishaji:** Ujumuishaji ni mchakato wa kuboresha jinsi ambavyo watu wanashiriki katika jamii, na kufikia huduma na rasilimali. Kujumishwa ni suala muhimu sana hasa kwa wanawake na wasichana anuwai ambao wanakabiliwa na ubaguzi, hatari kubwa na vizuizi zaidi vya kushiriki na kufikia huduma. Ujumuishaji unahusisha kushughulikia kwa ari, vizuizi na hatari ili kuhakikisha kila mtu anaweza kushiriki kwa njia ya maana na kufaidika kutokana na huduma. Ujumuishaji unahusisha kuongeza fursa, upatikanaji wa rasilimali, kujieleza na kusikika na kuheshimu haki.⁷
- **Utangamano wa vigezo:** Mfumo huu wa kitetea haki za wanawake uliobuniwa na Kimberlé Crenshaw⁸ unaelezea jinsi mifumo iliyoshikamana ya kukandamiza inamaanisha kuwa wanawake na wasichana wanakumbwa na dhuluma na ubaguzi kwa njia tofauti kulingana na mbari, daraja, umri, ulemavu, mwelekeo wa kingono, utambulisho wa kijinsia, kabila na dini yao. Njia inayozingatia utangamano inahitaji kuchukua hatua ili kufikia haki ya kijamii na inafaa ibuniwe kutokana na uelewaji wa matukio tofauti ya ukosefu wa usawa yanayowapata wanawake na wasichana, badala ya kupatia kipaumbele matukio au mahitaji ya kundi moja la wanawake juu ya lingine.
- **Uchache / Walio wachache:** Hakuna ufafanuzi uliokubaliwa kimataifa wa kuamua ni vikundi gani vinavyoweza kuitwa vya 'wachache'. Kwa jumla, wachache hufafanuliwa kama "vikundi tofauti ... kwa misingi ya kabila, dini au asili, na sehemu kubwa ya watu". Azimio la Umoja wa Mataifa la Wachache lililopitishwa mnamo 1992 linarejelea wachache kama vikundi kulingana na utambulisho wa kitaifa, kikabila, kitamaduni, kidini au lugha, na kusema kwamba nchi zinapaswa kuwalinda. Sifa zinazowatambulisha walio wachache hutofautiana sana kutoka muktadha mmoja hadi mwingine.⁹ La muhimu ni kwamba, vikundi vya kijamii havipendi kurejelewa kama "wachache" kwa sababu mtazamo huu unaweza kuhusishwa na "kuathirika kwa haraka", udhaifu au dhamana ya chini ilikinganishwa na walio wengi, hivyo kuamua uhusiano wa kimamlaka utakavyokuwa na kupuuza usawa. Kutokana na mtazamo huu hasi, Mwongozo huu unatumia neno 'kuhusishwa na kabila na dini fulani'.
- **Kushiriki: Kuwahusisha** wanawake na wasichana katika kufanya maamuzi na kuchukua hatua, kwa njia inayofaa, katika jamii zao na katika mfumo mpana wa utoaji misaada ya kibinadamu. Kushiriki kwa wanawake na wasichana huimarisha jamii zaidi kwa kujenga juu ya uwezo na rasilimali zilizopo za wanawake na wasichana anuwai. Kushiriki kwa wanawake na wasichana anuwai kutoka jamii iliyoathirika, wao binafsi na kupitia harakati na vikundi vya wanawake, kunaweza kuongeza uwezo na kuimarisha jamii husika, kuendeleza umiliki na kuboresha uendeleu.¹⁰ Kushiriki ni sehemu muhimu ya

Kwa mfano, huko Iraq na Syria, makundi ya jamii hayapendi kurejelewa kama 'ya wachache'. Wao hupinga kurejelewa vile kwa sababu:

- Msamiati ule unafanya waonekane kama wanaoweza kuathirika kwa haraka, hivyo kuonwa kana wanyonge au wasio na thamani ikilinganishwa na wengine.
- Dhana ile inaathiri husiano wa kimamlaka na kudhoofisha umoja miongoni mwa raia.
- Kwa baadhi ya makundi, dhana hii huonekana kuwa na maana zaidi ya historia yao kama watu asili au waliotoka eneo la Mesopotamia.

-Protection of Minorities in Iraq and Syria

⁷ WID, Where do we stand?

⁸ Demarginalizing the Intersection of Race and Sex: A Black Feminist Critique of Antidiscrimination Doctrine, Feminist Theory and Antiracist Politics, Kimberlé Crenshaw, 1989 <https://chicagounbound.uchicago.edu/cgi/viewcontent.cgi?article=1052&context=uclf>

⁹ UNHCR. Emergency Handbook, p. 1.

¹⁰ Action Aid, On the frontline: Catalyzing women's leadership in humanitarian action, p. 5 (2016).

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura
Mwongozo wa ujumuishaji

uwezesaji na huleta matokeo bora zaidi ya hatua zinazochukuliwa katika miktadha ya utoaji misaada ya kibinadamu.

- **Viwakilishi:** Kiwakilishi ni neno ambalo linarejelea anayezungumza (mimi au wewe) ama mtu au kitu kinachozungumziwa (yeye, wao, hiki au hii). Katika baadhi ya lugha, wanawake na wasichana waliobadili jinsia hutatizika wakati kiwakilishi wanachojitambulisha nacho hakilingani na jinsia waliyopewa walipozaliwa au mtazamo wa wengine wa utambulisho wao wa kijinsia. Kwa mfano, mwanamke aliyebadili jinsia anaweza kurejelewa kama 'he' katika Kiingereza na watu ambao hawajui kuwa anajitambulisha kwa jinsia ya kike na anapendelea kiwakilishi "she", ama pia watu ambao wanachanganywa na utambulisho wake wa kijinsia au wale wanaojaribu kumuumiza. Kuheshimu kiwakilishi cha mtu ni kitendo rahisi cha ujumuishaji.
- **Makao yanayofaa** yanarejelea marekebisho yanayohitajika na yanayofaa inapotakikana katika kesi fulani, na ambayo si mzigo mkubwa au usiofaa, kuhakikisha wanawake na wasichana wenye ulemavu wako sawa au wanaweza kufikia haki zote za binadamu na uhuru wa kimsingi kwa njia sawa na wengine.¹¹
- **Muundo/ufikiaji kwa wote** ni njia ya kuhakikisha ufikivu. Hii inamaanisha kuwa bidhaa, mazingira, mipango na huduma zinaundwa kwa njia ambayo zinaweza kutumiwa na watu wote, kwa kiwango kikubwa iwezekanavyo, bila haja ya kubadilishwa au kuwa na muundo maalum.

Vidokezo vya istilahi za kutumia na kuepuka

Kwa jumla, ikiwa huna uhakika utumie msamiati upi, ni muhimu kuuliza wanawake na wasichana wenyewe kuhusu lugha na maneno wanayopendelea, ikiwa ni pamoja na viwakilishi wanavyopendelea. Hapa tunashughulikia mwongozo wa jumla juu ya istilahi zinazofaa.

Jiepushe na kutaja watu ukitumia akronimi kwani zinaweza kuwabandika lebo. Pia jiepushe na kutumia 'mwingine/wengine', neno ambalo linashusha hadhi yao. Jiepushe na kumwelezea mtu kwa kutumia sifa moja tu, mfano, msagaji, mwanamke mlemavu.

Neno la kutumia	Neno la kuepuka ¹²
Wanawake na wasichana wenye ulemavu	Wanawake walemavu, PWD
Wanawake wazee	Wanawake waliozeeka, OAP
Wanawake na wasichana wenye mielekeo tofauti ya kingono na utambulisho tofauti wa kijinsia	Tomboy, lesbo, mwanamke-mwanaume, mvulana-mwanamke
wanawake na wasichana anuwai	Wanawake na wasichana waliotengwa
Ukatili wa kingono	Kulawiti, kunajisiwa

¹¹ [CRPD](#), Art. 2

¹² Avoid using acronym without full spelling: PWDs, Person with Disabilities; OAPs, Old Age Pensioners.

HATARI NA VIKWAZO VINAVYOWAKABILI WANAWAKE NA WASICHANA ANUWAI

Sehemu hii inaangazia hatari na vizuizi mahususi vya kijinsia vinavyowakabili wanawake na wasichana katika miktadha ya kibinadamu, ambavyo huzidishwa na vigezo vinavyotangamana vya ukosefu wa usawa. Sehemu hii kwanza inaorodhesha hatari na vizuizi vya kawaida ambavyo wanawake na wasichana wanaweza kukumbana navyo, kisha inaangazia hatari na vizuizi mahususi kwa vikundi tofauti vya wanawake na wasichana.

Ili kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia kwa njia bora, lazima tuelewe jinsi ukandamizaji kwa misingi ya umri, mbari, ulemavu, daraja, mwelekeo wa kingono, utambulisho cha kijinsia, kabila na dini, huongeza hatari na ubaguzi unaowakabili wanawake na wasichana anuwai katika miktadha ya dharura. **Wanawake na wasichana ambao wanakabiliwa na aina nyingi za kukandamizwa wako katika hatari kubwa ya kuathiriwa na unyanyasaji wa kijinsia na wanakabiliwa na vizuizi vingi katika kupata usaidizi na katika kupata nafuu.**

Wakati wahudumu wanaoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia wanajua hatari na vizuizi vinavyowakabili wanawake na wasichana anuwai, wanaweza kuchukua hatua ili kuviondoa na kuhakikisha kuwa wanawake na wasichana wote wanafikia huduma zinazoshughulikia unyanyasaji wa kijinsia. Pia wanaweza kuongeza uwezo wa mipango inayoshughulikia unyanyasaji wa kijinsia ili kujumuisha wanawake na wasichana anuwai katika jumuiya husika. Wahudumu wanaoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia wanaowajumuisha **wanawake anuwai kimakusudi katika timu zao** wataweza kuelewa na kuwasiliana na wanawake na wasichana anuwai katika jamii

“Leo hii, lazima changamoto yetu sisi na ya vuguvugu za wanawake ile kuweka uchangamano wa matukio tangamano ya ubaguzi wazi kiasi kwamba yanaonekana na yanaweza kuchukuliwa hatua ili wanawake waliotengwa wajumuishwe, sio tu kwa vile tunavyozungumza kuhusu kuleta mabadiliko, lakini pia kwa kuwashirikisha katika hatua ambazo tunaahidi kuendelea kuchukua kama vuguvugu za wanawake.”

Marsha Darling, AWID Forum “Reinventing Globalization” Guadalajara, Mexico, Ocktoba 2002

<https://www.awid.org/publications/intersectionality-tool-gender-and-economic-justice>

iliyoathiriwa na mzozo. Wahudumu wote wanaoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia wanaweza kujitolea kujifunza zaidi kuhusu uanuwai na utangamano wa vigezo mbalimbali na kuchukua hatua kuwajumuisha wanawake na wasichana wote.

Kuelewa jinsi nguvu na ufanyaji maamuzi ya wanawake na wasichana anuwai unavyopuuzwa zaidi na vigezo vya ukosefu wa usawa vinavyotangamana hivyo kuongeza hatari yao kuathiriwa na unyanyasaji wa kijinsia, kutasaidia wanaoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia kurekebisha jinsi wanavyokabiliana na visa hivi. Mambo ya kuzingatia ni pamoja na:

- **Taratibu za kupoteza usaidizi wa familia na jamii:** Wakati wa ufurushwaji, mara nyingi familia na jamii hutenganishwa na miundo ya kidesturi iliyo nguzo ya jamii inadhoofika. Udhaifu huu wa ulinzi wa jamii huathiri wanawake na wasichana anuwai kwa ukali zaidi kwani tayari wana njia chache za ulinzi na wana watu wachache zaidi wanaowaamini na wanaoweza kuwategemea ili kupata msaada ikiwa wanaathiriwa na unyanyasaji wa kijinsia. Katika muktadha wa dharura wanawake na wasichana wenye ulemavu, wasichana waliobalehe na wanawake wazee, wanaweza kutegemea wanafamilia au wanajamii wasiowajua sana jambo ambalo mara nyingi linaongeza hatari yao ya kudhulumiwa. Wanawake na wasichana wenye mwelekeo tofauti wa kingono na utambulisho tofauti wa kijinsia, hasa katika mazingira ambamo uhusiano wa jinsia moja ni hatia, wanaweza kuwa na mitandao na mikakati iliyobuniwa kwa uangalifu ya kutoroka kwao kwa njia salama zaidi kabla ya mzozo. Mitandao na mikakati hii husambaratishwa na ufurushwaji hivyo kuongeza hatari yao ya kuathiriwa na unyanyasaji wa kijinsia na kupunguza idadi ya watu ambao wanaweza kuwasaidia. Wanawake

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura
Mwongozo wa ujumuishaji

na wasichana kutoka makundi tofauti ya kidini na kikabila wanaweza kuwa katika hatari kubwa zaidi ya kuathiriwa na unyanyasaji wa kijinsia kwani wanaweza kuwa pia wamelengwa kwa sababu ya kabila au dini yao, hasa katika miktadha ambapo mizozo inatokana na sababu za kikabila au kidini.

- **Utegemezi na udhibiti:** Masuala ya nguvu na udhibiti yanaweza kuwa magumu zaidi katika mahusiano ambapo mwanamke au msichana hutegemea mzazi au mwenzi wake kama mlezi. Njia na mbinu za mamlaka na udhibiti ambazo zinaweza kutumiwa dhidi ya wanawake na wasichana anuwai wanaowategemea walezi ni pamoja na:¹³
 - Walezi wanaodhulumu wanaweza kutishia au hata kumnyima vipengele na msaada msingi wa utunzaji (chakula, pesa, usafi) au kumwacha peke yake.
 - Walezi wanaodhulumu wanaweza kutishia au kumnyima, kutumia vibaya au kuchelewesha usaidizi mahususi ambao ni msingi kwa mwanamke au msichana kuendeleza shughuli zake za kawaida (kwa mfano dawa, vifaa).
 - Walezi wanaodhulumu wanaweza kutumia pesa za mwanamke au msichana huyo kujinufaisha wenyewe na / au wafanye maamuzi ya kifedha kwa niaba yake bila kumwomba idhini.
 - Walezi wanaodhulumu wanaweza kumtenga mwanamke au msichana kutoka mitandao iliyopo katika jamii.
 - Walezi wanaodhulumu wanaweza kumdhidhaki na kumdhaliisha mwanamke au msichana kwa Walezi wanaodhulumu wanaweza kumlaumu mwanamke au msichana kama chanzo cha dhiki yao (k.m. kuwa inatokana na kuwatunza).

Uchambuzi wa vizuizi

Mfumo ufuatao wa uchambuzi wa vizuizi, uliotolewa kwenye uchambuzi wa vizuizi vya walemavu, unaweza kusaidia wanaoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia kutambua na kulenga vizuizi ambavyo vinaweza kuondolewa ili kuwasaidia wanawake na wasichana anuwai kufikia huduma na kushiriki.

Kimaumbile	Habari	Mitazamo	Taasisi
Vizuizi vya kimaumbile vinaathiri uwezo wa wanawake na wasichana anuwai kupata huduma na vinaweza kuwa vya asili au viwe vimetokana na watoa huduma katika miktadha ya kibinadamu au watoa huduma wengine. Vizuizi vya kimaumbile vinazidishwa na kanuni za kijinsia zinazozuia usafiri wa wanawake na wasichana na kufanya waathiriwa wa unyanyasaji wa kijinsia watengwe zaidi, jambo ambalo hufanya umbali wa vituo vya kutoa	Vizuizi vya habari hudhihirika wakati habari haitolewi na kuweza kufikiwa na wanawake na wasichana wote. Wanawake na wasichana wenye ulemavu wa kuona au kusikia, wanaozungumza lugha tofauti, na wanawake na wasichana ambao hawawezi kusoma vizuri, wote wanaweza kukabiliwa na changamoto kubwa ya kupata habari kuhusu huduma zinazoshughulika na visa vya unyanyasaji wa	Mitazamo inayodhuru inasalia kuwa mojawapo ya vizuizi vikuu vinavyowazuia wanawake na wasichana anuwai kushiriki kikamilifu na kwa njia sawa katika mipango inayoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia. Upendeleo usio wa kimaksudi au ubaguzi wa moja kwa moja huwazuia wanawake na wasichana anuwai kupata huduma na kushiriki katika mipango ya kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia.	Vizuizi vya kitaasisi ni taratibu na sera zinazobagua wanawake na wasichana anuwai. Kwa mfano, wakati idhini ya mwenzi wa kiume inahitajika ili kutoa huduma ya afya kwa walioathiriwa na unyanyasaji wa kijinsia. Jambo hili linabagua uhuru wa wanawake wa mwili na chaguo zake na linaweza kuwa kizuizi kikuu kwa wanawake katika uhusiano wa jinsia moja.

¹³ Interagency GBV Case Management Guidelines, p. 139. <https://gbvresponders.org/response/gbv-case-management/>, p. 141, citing Power & Control Wheel, Wisconsin Coalition Against DV.

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura
Mwongozo wa ujumuishaji

huduma jambo muhimu. kijinsia. Bila uwezo wa
Milango na ngazi kufikia habari wanawake
nyembamba, miteremko na wasichana hawawezi
iliyoinuka na kadhalika pia kufanya maamuzi
huwazuia wanawake na yanayofaa.
wasichana wenye
ulemavu wa kimwili
ambao wanatumia viti vya
magurudumu kufikia
huduma.



Vizuizi vya kimaumbile: Vizuizi vya kimaumbile vinaathiri uwezo wa wanawake na wasichana anuwai kupata huduma na vinaweza kuwa vya asili au viwe vimetokana na watoa huduma katika miktadha ya kibinadamu au watoa huduma wengine. Vizuizi vya kimaumbile vinazidishwa na kanuni za kijinsia zinazozuia usafiri wa wanawake na wasichana na kufanya waathiriwa wa unyanyasaji wa kijinsia watengwe zaidi, jambo ambalo hufanya umbali wa vituo vya kutoa huduma jambo muhimu. Milango na ngazi nyembamba, miteremko iliyoinuka na kadhalika pia huwazuia wanawake na wasichana wenye ulemavu wa kimwili ambao wanatumia viti vya magurudumu kufikia huduma. Wanawake na wasichana anuwai wanaweza kuwa wamefichwa au kutengwa na familia zao kwa misingi ya umri wa kubalehe, uzee au ulemavu, au huenda wakaficha utambulisho wao wakati kabila, dini, mwelekeo wao wa kingono au utambulisho wa kijinsia unaweza kuwaweka katika hatari ya kubaguliwa na kudhulumiwa. Kuishi kando na wengine huongeza zaidi hatari ya unyanyasaji wa kijinsia, hasa nyumbani, na hupunguza chaguo za wanawake na wasichana za kutafuta usaidizi. Kutengwa kunaweza kusababisha mfidhaiko na matatizo mengine ya kiakili, pia kunawazuia kufikia huduma za kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia, kunawazuia kujumuishwa tena katika fursa za kielimu na kiuchumi na kunawafanya wategemee wengine zaidi hivyo kunapunguza chaguo walizo nazo.

Habari: Vizuizi vya habari hudhihirika wakati habari haitolewi na kuweza kufikiwa na wanawake na wasichana wote. Wanawake na wasichana wenye ulemavu wa kuona, wanaozungumza lugha tofauti, na wanawake na wasichana ambao hawawezi kusoma vizuri, wote wanakabiliwa na changamoto kubwa za kupata habari iliyoandikwa kuhusu huduma zinazoshughulikia na visa vya unyanyasaji wa kijinsia. Aidha, habari ambayo inawatenga wanawake anuwai kwa kuonyeshwa tu aina fulani za wanawake wakipata huduma inakuwa kizuizi cha kufikia zile huduma kwa kufanya baadhi ya wanawake na wasichana kuhisi kuwa hawajakaribishwa au hawana uhakika kama wanaweza kupata huduma zile. Wanawake wenye ulemavu wa kusikia wanaweza kusumbuka kushiriki katika shughuli za nafasi salama na huduma zinazoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia ambapo lugha ya ishara haipatikani kuwasaidia kuwasiliana.

Mitazamo: Mitazamo inayodhuru inasalia kuwa mojawapo ya vizuizi vikuu vya kushiriki kikamilifu na kwa usawa kwa wanawake na wasichana katika mipango inayoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia. Upendeleo usio wa kimaksudi au ubaguzi wa moja kwa moja huwazuia wanawake na wasichana anuwai kupata huduma na kushiriki katika mipango ya kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia. Mitazamo inayompa mwanamume mamlaka katika familia na kubagua kwa misingi ya jinsia huwaathiri zaidi wanawake na wasichana anuwai ambao pia wanabaguliwa kwa misingi ya umri, kuwa mabasha na wabadili jinsia, kwa misingi ya mbari na ulemavu, daraja, hali ya VVU, dini na kabila na watoa huduma za kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia, wahudumu wengine katika miktadha ya kibinadamu wanafamilia na wanajamii. Ikiwa wahudumu wanaoshughulikia visa vya unyanyasi

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura
Mwongozo wa ujumuishaji

wa kijinsia hawachukui hatua ya kuwaeleza bayana wanawake na wasichana kuwa wamekaribishwa katika nafasi salama za wanawake na wasichana na mipango inayoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia, basi wanawake na wasichana hawa wanaweza kuhofia kuwa watakumbana na mitazamo inayodhuru sawa na iliyo kwenye jamii pana na huenda wakakataa kutafuta usaidizi.

Taasisi: Vizuizi vya kitaasisi ni taratibu na sera zinazobagua wanawake na wasichana anuwai. Kwa mfano, wakati idhini ya mwenzi wa kiume inahitajika ili kutoa huduma ya afya kwa walioathiriwa na unyanyasaji wa kijinsia, hii haibagui tu uhuru wa wanawake na uwezo wa kujichagulia, bali itakuwa kizuizi kikubwa kwa wanawake katika uhusiano wa jinsia moja. Wanawake na wasichana anuwai wanaowategemea sana wengine kama vile wasichana waliobalehe, wanawake na wasichana wenye ulemavu, au wanawake walioendelea kiumri, wanaweza kuhitaji kufichua hali yao kwa wengine ili kupata huduma, na watoa huduma au wanajamii wanaweza kuchukua hatua kwa niaba ya mwathirika bila idhini au kibali chake. Mifano mingine ambayo inaweza kusababisha kutengwa kwa wafanyikazi anuwai wa kike katika timu za wahudumu wanaoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia ni pamoja na, kanuni za kuajiri ambazo haziweza kubadilishwa au kurekebishwa kwa ajili ya wanawake wenye ulemavu, ambazo hazitoi nafasi kwa desturi tofauti za kidini, au hazitoi nafasi za utunzaji wa watoto au kuwapa wazazi nafasi ya likizo.

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura
Mwongozo wa ujumuishaji

Sehemu ifuatayo inaangazia vikundi tofauti vya wanawake na wasichana. Kutambua vikundi hivi mahususi vya wanawake na wasichana ni muhimu kama zana ya kupanga. Lakini, ni muhimu kutambua kwamba ni nadra sana kwa wanawake na wasichana kuwa katika kundi moja tu. Kwa sababu hii, ni muhimu kufikiria kuhusu tofauti za yale ambayo **kila** kikundi kimepitia na utangamano kati ya vikundi hivi. Kutazama wanawake na wasichana katika vikundi kulingana na hali moja ya utambulisho wao kunaweza kuficha kila moja ya hali zao maalum, ikiwemo nguvu zao.

Wasichana waliobalehe

Wasichana waliobalehe ni sehemu kubwa, na inayoendelea kuongezeka, ya watu waliofurushwa makwao. Wao wako katika hatari kubwa ya kubakwa, kufanyiwa ukatili wa kingono, ndoa za mapema na kutekwa nyara ikilinganishwa na vikundi vingine vya watu.¹⁴ Ushahidi unaonyesha kuwa wasichana waliobalehe wanakabiliwa na hatari nyingi wakati wa mzozo, na pia kwamba hawazingatiwi, hawalindwi na hawajumuishwi, hasa katika siku 45 za kwanza, ambazo ni muhimu.¹⁵ Wahudumu katika miktadha ya kibinadamu wasiposhughulikia wasichana waliobalehe wakati wa hali za dharura, uwezo wa wasichana hawa kupata kwa njia salama habari, huduma na nyenzo wanazohitaji za kujiokoa hubanwa.¹⁶

Girl Shine, mpango na nyenzo inayolenga kusaidia, kulinda na kuwezesha wasichana waliobalehe katika miktadha ya dharura, ina maelekezo mahususi ya jinsi ya kushirikisha wasichana hawa katika kuandaa, kutekeleza na kufuatilia mipango ya kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia iliyobuniwa kwa ajili ya wasichana waliobalehe.

Wasichana wenye umri wa miaka 10 hadi 14 na wale wakubwa wenye miaka 15 hadi 19 ni miongoni mwa sehemu ya watu walio hatarini zaidi katika miktadha ya kibinadamu; yaani wanahitaji ulinzi zaidi lakini ni mojawapo ya makundi ya watu waliotelekezwa zaidi.¹⁷ Wanapoingia umri wa kubalehe, wasichana hawa wadogo huanza kuchukua kazi na majukumu ya watu wazima, ingawa bado hawana ustadi au uwezo wote wa mwili na utambuzi ambao wanahitaji.¹⁸

Wasichana waliobalehe hukabiliwa na hatari kubwa ya unyanyasaji wa kijinsia na vizuizi zaidi vya kupata huduma kwa sababu ya mambo yafuatayo:

- Kaida za jamii na utamaduni zimetengenezwa kwa njia inayowezesha kugandamiza na kutawala wasichana waliobalehe.
- Taasisi dhaifu, umaskini na ugumu wa kifedha huwacha wasichana katika hatari ya unyanyasaji, unyonyaji na dhuluma (ikiwa ni pamoja na uchumaji hatari wa riziki).
- Vizuizi vya kutembea huru na kuona huwatengwa wasichana hawa zaidi, huvunja uhusiano wao na marafiki na kuwatenga na mitandao mingine ya kuwasaidia.
- Uwezo finyu wa kupata habari na huduma zinazowafaa vijana unaathiri maisha ya wasichana waliobalehe.
- Wahudumu katika miktadha ya kibinadamu kutozingatia kwa makini majukumu, mahitaji na hatari za kipekee zinazowakumba wasichana waliobalehe.¹⁹

¹⁴ COMPASS Learning Report: "A Safe Place to Shine: Creating Opportunities and Raising Voices of Adolescent Girls in Humanitarian Settings" <https://gbvresponders.org/compass/>; WRC, I'm Here, p. 5.

¹⁵ The Girls in Emergencies Collaborative, Statement and Action Agenda from the Girls in Emergencies Collaborative, September 2015, p. 2. <https://www.popcouncil.org/research/statement-and-action-agenda-from-the-girls-in-emergencies-collaborative>

¹⁶ I'm Here: Adolescent Girls in Emergencies, Women's Refugee Commission, 2014, p. 12.

¹⁷ I'm Here: Adolescent Girls in Emergencies, Women's Refugee Commission, 2014, p. 17.

¹⁸ Adolescent Sexual and Reproductive Health Toolkit for Humanitarian Settings, UNFPA, 2009, p. 6. <https://www.unfpa.org/publications/adolescent-sexual-and-reproductive-health-toolkit-humanitarian-settings>

¹⁹ WRC, I'm Here: Adolescent Girls in Emergencies, Women's Refugee Commission, 2014, p. 22.

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura Mwongozo wa ujumuishaji

Mipango jumuishi ya kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia hutofautisha kati ya mahitaji ya wasichana wadogo na wale wa umri wa juu zaidi ambao wanakabiliwa na changamoto, hatari na ubaguzi wa kipekee wanapoendelea kukomaa.²⁰ Sharti wahudumu wanaoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia watambue kuwa wasichana waliobalehe si kundi linalovutiwa na jinsia tofauti pekee na wajitolee kuona "ulimwengu" kamili wa wasichana,²¹ wenye tofauti zikiwemo umri (vijana wa miaka 10-16, vijana wa miaka 15-19), hali ya ndoa, wenye walezi au mayatima, hali ya VVU, kabila, wanaoenda na wasioenda shule na wasio na kazi, wasio na wakati, wajawazito au wanaonyonyesha, walemavu, wenye watoto au wanaowachunga wengine, mwelekeo wa kingono, utambulisho wa kijinsia na wale ambao ni waathiriwa wa ukatili wa kingono.^{22 23} Wahudumu wanaoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia wanapaswa kujitolea kutoa utunzaji na huduma kwa huruma. Pia zinafaa ziwe zinazopatikana, zinazokubalika na zinazofaa kwa wasichana anuwai, wadogo na wakubwa.²⁴

Wasichana wengi waliobalehe – ambao ndio maskini zaidi katika jamii maskini – tayari wanaishi katika hali ya “dharura”. Mizozo ya kibinadamu huangazia tu zaidi haja yao ya kuweza kukabiliana na hali yao na kupata utunzaji, huku ikiwazidishia hatari ya kudhulumiwa.

Collaborative for Girls in Emergencies, Statement

²⁰ Girl Shine Program Model: <https://gbvresponders.org/adolescent-girls/girl-shine/>

²¹ The Protective Asset-Building Approach, in Building Girls' Protective Assets, PopCouncil, 2016, p. iv.

²² Adolescent Sexual and Reproductive Health Program in Humanitarian Settings: An In-depth Look at Family Planning Services, WRC 2012, p. 24.

²³ WRC, I'm Here: Adolescent Girls in Emergencies, Women's Refugee Commission, 2014, p. 17.

²⁴ WHO Global Consultation in 2001 and discussions at a WHO expert advisory group in Geneva in 2002. Noted in: Adolescent-friendly Health Services: An Agenda for Change, WHO 2002, p. 27. <https://apps.who.int/iris/handle/10665/67923>

Wanawake waliokomaa zaidi

Chuki iliyokita mizizi dhidi ya wanawake ambao ni uzee huendeleza ubaguzi kwa misingi ya umri na kuendeleza tabia za kijamii ambazo zinakubali au hata kuendeleza unyanyasaji, dhuluma na kutelekezwa kwa wanawake katika uzee wao.²⁵ Kufikia 2050, idadi ya watu wazee ulimwenguni itazidi idadi ya vijana kwa mara ya kwanza katika historia. Idadi hii itakuwa asilimia 22 ya idadi ya watu wote duniani.²⁶ Idadi kubwa ya watu wazee wataendelea kuwa wanawake wanaoishi katika nchi za kipato cha chini au cha kati na ambao watakuwa wengi kuliko wanaume kadri wataavyoendelea kuzeeka. Katika mwaka wa 2015, asilimia 54 ya idadi ya watu wenye umri wa miaka 60 kwenda juu na asilimia 61 ya idadi yote ya watu ulimwenguni wenye miaka 80 au zaidi ilikuwa wanawake.²⁷ Wanawake wenye umri wa miaka 50 kwenda juu wanawakilisha karibu robo moja (asilimia 23.6) ya wanawake ulimwenguni kote.²⁸

Wanawake ambao ni wazee wanaweza kuwa wameathiriwa na unyanyasaji wa kijinsia maisha yao yote, ingawa aina fulani za unyanyasaji zinaweza kutokea zaidi uzeeni. Sheria na desturi za kibaguzi dhidi ya wanawake ambao ni wazee katika nyanja zote za maisha yao ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na familia huendeleza dhuluma na unyanyasaji.²⁹ Ulimwenguni kote, karibu nusu ya wanawake ambao ni wazee wanaishi peke yao kwa sababu ya kuwa wajane, kupewa talaka au hawakuwahi kuolewa. Hatari ya wanawake wazee ambao wametengwa na marafiki, familia, na jamii kunyanyaswa, kukosa au kuwa na uwezo finyu wa kupata huduma au msaada iwapo watanyanyaswa au kudhulumwa huwa juu mara tatu³⁰.

Unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya wanawake ambao ni wazee umeenea ingawa bado umejificha. Ripoti ya Shirika la Afya Duniani ya Makadirio ya Ulimwenguni na ya Kikanda ya Dhuluma dhidi ya Wanawake (2013), ilipata kuwa kiwango cha dhuluma inayodumu inayotekelezwa na wenzi miongoni mwa wanawake wenye zaidi ya miaka 50 kilikuwa asilimia 20.6. Kiwango hiki kulichoripotiwa chaweza kuwa chini ya hali halisi kwa sababu si mengi yanayojulikana kuhusu ruwaza za unyanyasaji dhidi ya wanawake ambao ni wazee ikilinganishwa na wale walio na umri wa miaka 15-49.³¹ Unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya wanawake ambao ni wazee hujitokeza katika aina nyingi, mara nyingi ukijumuisha aina zinazoendelezwa na wenzi, wanafamilia (wakiwemo watoto waliokomaa wa kike na wa kiume), walezi au jamii pana. Wanawake wengi ambao ni wazee hupitia aina moja au zaidi ya dhuluma, utelekezaji na unyanyasaji wa mwili, kingono, kifedha na kisaikolojia. Kwa wanawake wazee ambao wameathiriwa na unyanyasaji wa kingono, athari za kiafya na majeraha yanayotokana na unyanyasaji huo huwa makali zaidi.³² Kuna ushahidi mwingi unaoonyesha kwamba uzee huathiri tabia ya wanawake kutafuta huduma za afya na upataji huduma kwa jumla, jambo ambalo linamaanisha kuwa athari hatari za kiafya zinazotokana na unyanyasaji wa kijinsia zinawezakosa kutibiwa na zinaweza kuzidi, na kwamba unyanyasaji huu huendelea na unaweza kuongezeka kwa mara na ukali. Kwa asilimia fulani, kwa sababu mara nyingi wanawake wanaozingatiwa ni wale wa umri wa kuzaa, afya ya kingono ya wanawake ambao ni wazee huwa mara nyingi imepuuzwa, kutengwa na kuonekana kama suala la aibu, hivyo kuzuia upatikanaji wa huduma za kuinga na za utunzaji wa waathiriwa na dhuluma na magonjwa ya zinaa, yakiwemo VVU. Watoa huduma wengi huepuka kuongea na

²⁵ Ibid.

²⁶ ADCAP Training, p. 17. <https://www.helpage.org/what-we-do/emergencies/adcap-age-and-disability-capacity-building-programme/>

²⁷ VAWG Resource Older Women, p. 2-3.

²⁸ Ibid

²⁹ United Nations General Assembly. (2013). Follow-up to the International Year of Older Persons: Second World Assembly on Ageing: Report of the Secretary General (A/68/167).

³⁰ VAWG Resource Older Women, pgs. 7-8.

³¹ HelpAge International, Violence against Older Women Discussion Paper 2017, p. 1. <https://www.helpage.org/what-we-do/rights/violence-against-older-women/>

³² VAWG Resource Older Women, p. 9.

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura
Mwongozo wa ujumuishaji

wagonjwa wao juu ya afya ya ngono (kwa sababu kadhaa kama kutokuwa na wakati, ukosefu wa rasilimali, mafunzo au uwezo) na uwezekano wao wa kuuliza wagonjwa wazee maswali juu ya shughuli za ngono ni finyu zaidi.³³

Idadi kubwa ya wanawake wazee wenye shida ya akili hudhulumiwa kwa njia moja au nyingine, na shida walio nayo ya akili inaweza kuwazuia kutafuta usaidizi.³⁴ Ulemavu unaweza kuwa hatari nyingine kwa wanawake ambao ni wazee, ambao huenda wakapata ulemavu unaohusiana na umri. Ulimwenguni kote, zaidi ya asilimia 46 ya watu wenye umri wa miaka 60 kwenda juu wana ulemavu, wengi wao wakiathiriwa na matatizo ya kuona na kusikia.³⁵ Wanawake wenye ulemavu wa maisha wanaweza kuathiriwa zaidi na dhuluma kadri wanavyozeeka, hasa ikiwa wanategemea mtu mwingine kwa utunzaji wa kila siku.³⁶

Wanawake wazee wanaweza kuwa katika hatari kubwa ya unyanyasaji wa kijinsia kwa sababu ya kupungua kwa nguvu na hadhi baada ya kuishi maisha yenye fursa chache za usalama wa kiuchumi na za elimu kwa sababu ya jinsia yao.³⁷ Ubaguzi kwa misingi ya umri na jinsia kwa pamoja unaweza kuongeza uwezekano wa umaskini, kupunguza uwezo wa kufikia nyenzo za ulinzi na kuongeza hatari ya unyanyasaji wa kijinsia.

“Uzee” na Ubaguzi kwa Misingi ya Umri

Hakuna makubaliano duniani kote kuhusu wakati “uzee” unaanza kwa sababu sana sana mtazamo wa kuzeeka hubadilika kulingana na mtu binafsi, jamii na miktadha ya kijamii.

Ubaguzi kwa misingi ya umri ni kasumba za kimfumo na ubaguzi dhidi ya watu kwa sababu wanachukuliwa kuwa ni wazee. Mtazamao wa uzee unachangiwa pakubwa na ubaguzi kwa misingi ya umri, jambo linaloweza kuzuia zaidi juhudi za kufikia usawa kw ajili ya wanawake wazee.

VAWG Resource Older Women

Wanawake ambao ni wazee hubaguliwa kwa sababu ya mitizamo na kaida zinazowapa wanaume mamlaka na ambazo zinaupa ujana na jukumu la wanawake la kuzaa watoto kipaumbele. Ubaguzi huu unaweza kufanya wanawake ambao ni wazee kuonekana kama “wasio na maana” au waonekane kama wasio na thamani mara tu wanapopitisha umri wa kutopata watoto. Hali hii inazua aina mahususi ya hatari ya kudhulumiwa inayotokana na uzee na jinsia.³⁸ Huduma zinazotolewa katika miktadha ya kibinadamu zinashughulikia wanawake wa umri wa “kupata watoto”, dhihirisho tosha la utangamano kati ya ubaguzi kwa misingi ya umri na ya jinsia ambao huwafunga wanawake katika jukumu lao tu la kupata watoto na wao huhesabiwa kama “wanawake” kulingana na uwezo wao wa kuzaa. Kulingana na shirika la HelpAge International, iwapo mtazamo huu hautajaribu kubadilishwa, basi huenda ukaendelea kasumba hatari kuwa dhuluma hutokea tu kwa vijana na kutenga yale wanayopitia wanawake wazee.³⁹

Sawa na wasichana waliobalehe, mizozo ya kibinadamu inaweza kuongeza zaidi hatari zinazowakabili wanawake wazee, kwa sababu vidhibiti vya kawaida vya kijamii huharibiwa. Kwa mfano, katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, asilimia 15.5 ya wanawake waliofika hospitalini ya Kivu Kusini kutafuta matibabu baada ya kupitia ukatili wa kingono kati ya 2004 na 2008 walikuwa na umri wa miaka 55 kwenda juu. Ripoti kutoka Iraq zilionyesha kaburi kubwa la wanawake wazee wa Yazidi waliouawa na serikali za Iraq na Syria; kulingana na wahudumu wa kibinadamu wanaowasaidia wanawake wachanga walionusurika, wanawake wenye umri wa miaka 40 kwenda juu

³³ VAWG Resource Older Women, p. 5.

³⁴ VAWG Resource Older Women, pgs. 7-8.

³⁵ ADCAP Training, p. 18. <https://www.helpage.org/what-we-do/emergencies/adcap-age-and-disability-capacity-building-programme/>

³⁶ VAWG Resource Older Women, pgs. 7-8.

³⁷ VAWG Resource Older Women, p. 4.

³⁸ VAWG Resource Older Women, p. 3.

³⁹ HelpAge International, Violence against Older Women Discussion Paper 2017, p. 3.

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura
Mwongozo wa ujumuishaji

Asilimia 32 ya wanawake wenye zaidi ya miaka 49 walidhulumiwa na wapenzi wao (asilimia 17 katika mwaka uliopita), huku **asilimia 37** walidhulumiwa na **na watu wengine wasio wapenzi wao** (asilimia

waliuawa kwa sababu hawangenunuliwa na kuuzwa kama watumwa wa ngono.⁴⁰ Uchunguzi uliohusisha wanawake wazee waliosemekana kuwa wachawi huko Burkina Faso unaonyesha athari nyingi za afya ya akili zinazotokana na kukataliwa na jamii. Asilimia 55 ya wanawake waliohojiwa walidokeza kwamba wazo lao la kwanza walipotuhumiwa lilikuwa kujiua.⁴¹

⁴⁰ VAWG Resource Older Women, p. 8.

⁴¹ VAWG Resource Older Women, p. 9.

Wanawake na wasichana wenye ulemavu

Duniani kote, takriban asilimia 15 ya wanawake na wasichana wana ulemavu⁴² na asilimia hii huongezeka katika miktadha ya kibinadamu ambapo mizozo na / au majanga ya asili husababisha visa mpya vya ulemavu kutokana na majeraha na uwezo finyu wa kufikia huduma za afya. Wanawake na wasichana wa kila kizazi wenye ulemavu wanakabiliwa na dhuluma na unyanyasaji kwa viwango ambavyo vinafikia asilimia 80 katika maisha yao.⁴³ Wanawake na wasichana wenye ulemavu katika miktadha ya kibinadamu wanakabiliwa na vizuizi zaidi vya kujikinga dhidi ya madhara, wanategemea wengine ili kuishi, hawana nguvu na hawazingatiwi.⁴⁴

Wanawake na wasichana wenye ulemavu wanakumbwa na hatari na vizuizi vingi zaidi katika miktadha ya kibinadamu kwa kuwa wametenganishwa na familia, wamepoteza vifaa vya kuwasaidia na vya kutembea na pia wanatatizika kupata habari. Wamo katika hatari zaidi ya kunyanyaswa na kudhulumiwa na ni miongoni mwa vikundi vya kijamii vilivyotengwa katika jamii yoyote iliyoathiriwa na mzozo. Wao wanaweza kutatizika kufikia mipango ya usaidizi wa kibinadamu kutokana na vizuizi mbalimbali vya kijamii, kimazingira na kimawasiliano.

Wanawake na wasichana wenye ulemavu huwa hawaathiriwi zaidi na dhuluma kwa sababu ya ulemavu walio nao, wanaathiriwa zaidi kwa sababu wanaonekana tofauti, hawana nguvu nyingi, wamepewa hadhi ya chini na wametengwa. Sababu hizi hufanya wanaoendeleza dhuluma walengwe zaidi.

Kwa wanawake na wasichana wenye ulemavu, utangamano wa vigezo vya ukosefu wa usawa wa kijinsia na ulemavu huwafanya wawe katika hatari kubwa ya unyanyasaji wa kijinsia. Ripoti ya mwaka 2015 ya ujumuishaji wa walemavu nchini Burundi, Ethiopia, Jordan na Caucasus ya Kaskazini, inasema kwamba ukatili wa kingono ndio aina ya unyanyasaji wa kijinsia iliyoripotiwa zaidi na washiriki wa vikundi vya utafiti katika muktadha wa mradi huo. Baadhi ya wanawake na wasichana wenye ulemavu waliripoti kulipitia ukatili wa kingono, ikijumuisha ubakaji uliojirudia, wa mara kwa mara na uliofanywa na watu wengi. Familia na watoa huduma wanaweza tu kufahamu kuhusu ukatili wa kingono dhidi ya wanawake na wasichana wenye ulemavu wanapokuwa wajawazito.⁴⁵ Kumekuwa na ripoti za ndoa za watoto miongoni kwa wasichana wenye ulemavu ambao huenda wakashinikizwa waolewe mapema kabla hawajaanza kutambuliwa kama "wasiofaa" kwa sababu ya umri wao na ulemavu.⁴⁶ Huenda waathirika wenye ulemavu wakangojea zaidi ya mwezi mmoja kabla ya kuripoti kisa cha dhuluma, kwa sababu ya vizuizi vingine vinavyowazuia kufichua.⁴⁷

Wanawake na wasichana wenye ulemavu wanaweza kukabiliwa na vizuizi vya kipekee katika kupata huduma zinazoshughulikia unyanyasaji wa kijinsia na kushiriki katika mipango inayoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia. Vizuizi hivi vinajumuisha:

- **Vizuizi vya kimaumbile** : Hivi vinaweza kuwa vya asili au vilivyobuniwa na watu. Vizuizi vya kawaida ni pamoja na milango na njia nyembamba, ngazi, mabadiliko ya ghorofa, miteremko isiyo na usawa na yenye miinuko, vyoo vya umma visivyoweza kufikiwa, taka na uchafu, mgawo wa chakula kizito, na huduma, maji na kuni zilizo mbali. Vizuizi hivyo vya kimaumbile huwazuia wanawake na wasichana kushiriki kikamilifu

⁴² Interagency GBV Case Management Guidelines, p. 139. <https://gbvresponders.org/response/gbv-case-management/>

⁴³ VAWG Resource Older Women, pg. 7-8.

⁴⁴ IRC/WRC 2015. Building Capacity for Disability Inclusion in Gender-Based Violence Programming in Humanitarian Settings: A Toolkit for GBV Practitioners, p. 5. <https://gbvresponders.org/response/disability-inclusion-2/>

⁴⁵ IRC/WRC 2015. Building Capacity for Disability Inclusion in Gender-Based Violence Programming in Humanitarian Settings: A Toolkit for GBV Practitioners, p. 5. <https://gbvresponders.org/response/disability-inclusion-2/>

⁴⁶ IRC/WRC 2015. Building Capacity for Disability Inclusion in Gender-Based Violence Programming in Humanitarian Settings: A Toolkit for GBV Practitioners, p. 5. <https://gbvresponders.org/response/disability-inclusion-2/>

⁴⁷ IRC/WRC. 2015.

katika maisha ya jamii au kupata huduma wanazohitaji. Huduma za kuzuia na kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia zinaweza kosa kufikiwa kwa sababu ya umbali, ukosefu wa mbinu za usafiri zinazofikika au gharama zinazohusiana na kufika pale. Isitoshe, huenda zahanati na vituo vya wanawake viwe tatizo kufikia kwa watumiaji wa viti vya magurudumu au wengine wenye changamoto zingine za kusafiri, jambo ambalo pia linaweza kutoa ujumbe kwamba wanawake na wasichana wenye ulemavu hawakaribishwi kupokea huduma zile.

- **Mawasiliano.** Huenda habari kuhusu huduma za kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia hazijatolewa kwa namna ambapo zinaweza kufikiwa na wanawake na wasichana wenye ulemavu, wakiwemo wale wenye ulemavu wa kuona, kusikia na akili au kisaikolojia. Kutokana na hayo, huenda wanawake na wasichana wenye ulemavu, hasa wale wenye ulemavu wa akili, wasitambue unyanyasaji pindi unapotokea au labda hawajui wapi pa kupata msaada. Aidha, watoa huduma katika visa vya unyanyasaji wa kijinsia wanahitaji kutambua mitindo na aina tofauti za mawasiliano ya kibinafsi na kuhudumia mwanamke na msichana mwenye ulemavu kwa kutumia mtindo wake maaluma wa mawasiliano. Kutenga muda na kumakinika ili kutambua lugha ya mwanamke au msichana fulani kunaweza kuhitaji msaada kutoka kwa mwanafamilia au rafiki ambaye si mnyanyasaji.
- **Uhusiano na walezi.** Huenda wanawake na wasichana wenye ulemavu wakawategemea wanafamilia au wanajamii wengine ili kupata huduma na usaidizi, jambo ambalo linafanya iwe vigumu kwao kupata huduma kwa njia ya siri. Ikiwa mlezi ndiye mnyanyasaji, itakuwa vigumu sana kwa mwathiriwa kupata msaada kwa sababu yeye anamategemea mlezi kwa mawasiliano, usafirishaji na mahitaji ya kila siku.
- **Hofu ya kutoaminiwa.** Kama ilivyo kwa waathirika wote wa unyanyasaji wa kijinsia, kizuizi cha kawaida katika kufikia huduma ni hofu ya mwathiriwa kwamba hakuna atakayemwamini. Changamoto hii inaongezeka zaidi kwa waathiriwa walemavu, hasa wale wenye ulemavu wa akili, ambao ufahamu na uwezo wa kufanya maamuzi unaweza kutiliwa shaka kwa njia isiyofaa. Waathiriwa hawa wanaweza kuogopa kwamba hakuna atakaye waamini ikiwa watamwambia mtu, jambo ambalo linaweza kuwaweka katika hatari zaidi ya kudhulumiwa.
- **Mtazamo juu ya uwezo wa wanawake na wasichana wenye ulemavu.** Huenda watu wasiwasikilize wanawake na wasichana wenye ulemavu au hata kuwaamini wanapofichua kuwa wamedhulumiwa, hasa ikiwa mwathiriwa ana ulemavu wa akili au kisaikolojia. Isitoshe, huenda wanawake na wasichana wenye ulemavu wakanyimwa fursa za kujifunza kuhusu dhuluma, ngono na uhusiano mzuri, na kupata ujuzi mpya na kuimarisha mitandao ya rika. Hivyo, wanaweza kulengwa katika visa vya ubakaji, dhuluma na unyanyasaji, au wawe na uwezo finyu wa kujitetea katika uhusiano wa kimapenzi.

Wanawake na wasichana walio na mwelekeo tofauti wa kingono na utambulisho tofauti wa kijinsia

Vurugu na ubaguzi dhidi ya wanawake na wasichana wenye mwelekeo tofauti wa kingono na utambulisho tofauti wa kijinsia umeenea sana ulimwenguni kote na huongezeka katika miktadha ya ufurushwaji na mizozo. Wanawake na wasichana walio na mwelekeo tofauti wa kingono na utambulisho tofauti wa kijinsia wanakabiliwa na hatari na vizuizi vingi kutokana na kaida zinazompa mwanamume mamlaka katika familia, kaida za jamii zinazoeneza chuki dhidi ya mabasha na wabadili jinsia, ukosefu wa usawa katika mifumo na vurugu. Wanawake na wasichana walio na mwelekeo tofauti wa kingono na utambulisho tofauti wa kijinsia wanaweza kuwa na mitandao na mikakati waliyobuni kwa uangalifu ya kutoroka kwao kwa njia salama zaidi, lakini mitandao na mikakati hiyo huvurugika wakati wa ufurushwaji hivyo kuwaongezea hatari ya kuathiriwa na unyanyasaji wa kijinsia. Mara nyingi watoa huduma katika miktadha ya kibinadamu huwa na mtazamo wa kawaida wa jinsia na hutoa huduma kwa misingi ya dhana kuwa wanaume ndio viongozi wa kaya au wanawake na wasichana wana washirika wa kiume. Huenda watoa huduma katika miktadha ya kibinadamu wakawa na chuki dhidi ya mabasha au wabadili jinsia na kuwatenga kimaksudi wanawake na wasichana wenye mwelekeo tofauti wa kingono na utambulisho tofauti wa kijinsia wakati wa kutoa huduma.

Wanawake na wasichana wenye mwelekeo tofauti wa kingono na utambulisho tofauti wa kijinsia mara nyingi hulengwa katika kila aina ya unyanyasaji wa kijinsia kwa sababu ya mwelekeo wa kingono na utambulisho wao wa kijinsia. Unyanyasaji huu ni pamoja na ukatili wa kingono, kudhulumiwa na wapenzi, ndoa ya kulazimishwa, unyanyasaji wa kimwili na kimihemko na kunyimwa nyenzo, huduma na fursa. Wanawake na wasichana wasenge, wanaoshiriki ngono na jinsia zote mbili na waliobadili jinsia wanaweza kukabiliwa na unyanyapaa mkubwa katika upataji huduma kwa sababu mwelekeo wao wa kingono au utambulisho wao wa kijinsia haujakubalika na familia zao, jamii na watoa huduma. Ili kukabiliana na kukataliwa na kubaguliwa na kijamii, wanawake na wasichana wenye mwelekeo tofauti wa kingono na utambulisho tofauti wa kijinsia wanaweza kuficha utambulisho wao na huenda wasifichue mahitaji waliyo nayo au huenda wasitafute msaada.

Wanawake na wasichana walio na mwelekeo tofauti wa kingono na utambulisho tofauti wa kijinsia wamo katika hatari kubwa ya aina nyingi za dhuluma kutoka kwa wenzao, wanafamilia, majirani au wapenzi. Katika kiwango cha familia, ubaguzi na dhuluma dhidi ya wasichana na wanawake wenye mwelekeo tofauti wa kingono na utambulisho tofauti wa kijinsia zinaweza kutoka kwa vyanzo vitatu vinavyohusiana: 1) shinikizo kubwa la kuolewa na kuwa na uhusiano na jinsia tofauti, 2) wanafamilia wanaodhulumu kujaribu kulazimisha tabia ya kawaida za jinsia kulingana na kaida za kijinsia zisizobadilika, na 3) kutenganishwa na kutengwa na familia na nyenzo za jamii.⁴⁸ Dhana ya "ubakaji ili kurekebisha" wanawake ni desturi ambayo hujaribu "kuponya" mwanamke msagaji au mwenye uhusiano na jinsia zote mbili kwa kumlazimisha kufanya ngono na mwanaume au wanaume wengi.

⁴⁸ VAWG Resource GM, p. 5.

Jinsia, mwelekeo wa kingono na utambulisho wa kijinsia ni sifa msingi za binadamu. Haki ya mtu kujitambulisha kwa jinsia yake, mwelekeo wake wa kingono na utambulisho wake wa kijinsia bila woga au adhabu ni sehemu msingi ya heshima kwa binadamu.

Unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya wanawake na wasichana wenye mwelekeo tofauti ya kingono na utambulisho tofauti wa kijinsia hukusudia kuendeleza nafasi tawala ya wanaume wanaovutiwa na jinsia tofauti katika jamii.⁴⁹

Sheria baguzi mara nyingi hupiga marufuku uhusiano wa kimapenzi wa jinsia moja na tabia zisizoambatana na mwelekeo wa kawaida wa kijinsia. Baadhi ya athari za sheria hizi ni kushtakiwa kwa kuwa na uhusiano wa kimapenzi na na jinsia moja na kuongeza hatari ya wanawake na wasichana kulengwa na polisi ili kutozwa hela kwa nguvu na kuvurugwa, au kudhulumiwa na wanajamii kwa kutishwa kuwa wataripotiwa kwa polisi kuwa wana uhusiano wa kimapenzi na jinsia moja. Sheria za familia na za jumla zinazobagua zinaweza pia kuathiri ustawi wa wanawake na wasichana wenye mwelekeo tofauti wa kingono na utambulisho tofauti wa kijinsia. Sheria hizi ni pamoja na ufafanuzi wa serikali wa familia na ndoa, kwa mfano, na pia uwezo wa mtu

kubadilisha jinsia aliyopewa wakati wa kuzaliwa katika hati rasmi za serikali.⁵⁰

Wanawake na wasichana walio na mwelekeo tofauti wa kingono na utambulisho tofauti wa kijinsia wanaweza kukabiliwa na vizuizi vingi vya kuishi bila kuficha au "kutangaza rasmi" kwa marafiki, familia na jamii zao kwa kuhofia uhasama, kukataliwa au unyanyasaji ikiwa watashiriki utambulisho wao. Iwapo watoa huduma katika visa vya unyanyasaji wa kijinsia hawatawakaribisha na kuwajumuisha wazi, basi wanawake hawa watakabiliwa na vizuizi sawa wakati wa kutafuta huduma na huenda wakaogopa kuwa hawajakaribishwa katika nafasi salama za wanawake na wasichana au mipango inayoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia. Wakati watoa huduma katika visa vya unyanyasaji wa kijinsia wanashikilia mtazamo wa kawaida wa jinsia na kuchukulia kuwa wanawake na wasichana wanajitambulisha kwa jinsia waliozaliwa nayo, basi wao huweka vizuizi ambavyo wanawake na wasichana wasenge, wanaoshiriki ngono na jinsia zote mbili na waliobadili jinsia wanapaswa kukabiliana navyo. Wanawake na wasichana wasenge, wanaoshiriki ngono na jinsia zote mbili na waliobadili jinsia wanakabiliwa na hatari kubwa ya unyanyasaji wa kijinsia, viwango vya juu vya kukataliwa na familia na jamii zao, mitandao michache ya msaada katika jamii na nafasi chache za elimu na kujikimu kiuchumi. Kwa kuwa wao wanahitaji sana huduma zinazoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia na hawana njia mbadala za usaidizi katika jamii au hata mali nyingi, basi ni muhimu mipango inayoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia iwajumuishe na kuwakaribisha wanawake na wasichana wasenge, wanaoshiriki ngono na jinsia zote mbili na waliobadili jinsia.

Viwakilishi nafsi (mahususi kwa baadhi ya lugha kama Kiingereza):

Kiwakilishi nafsi ni neno linalorejelea anayezungumza ('I' au 'you') au anayezungumziwa/kinachozungumziwa (she, he, it, them au this). Wabadili jinsia hutatizika wakati kiwakilishi kinachotumika kuwarejelea hakiambatani na jinsia waliyopewa walipozaliwa au jinsia ambayo wengine wanawatambulisha nayo. Kwa mfano, mwanamke aliyebadili jinsia anaweza kurejelewa kwa kiwakilishi nafsi "he" na watu ambao

⁴⁹ VAWG Resource GM, p. 6.

⁵⁰ VAWG Resource GM, p. 6.

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura
Mwongozo wa ujumuishaji

Baadhi ya changamoto ambazo zinawakabili wanawake na wasichana walio na mwelekeo tofauti wa kingono na utambulisho tofauti wa jinsia ni pamoja na:

- Kutoamini walio mamlakani kutokana na kulengwa na polisi na viongozi wengine.
- Woga kuwa familia zao zitajua wakishiriki hali yao na mashirika ya kibinadamu.
- Woga kuwa wafanyikazi wanaotoa misaada ya kibinadamu watawabagua au kuwachukulia kwa mtazamo fulani bila kuthibitisha.
- Imani kuwa kushiriki utambulisho wao kunaweza kuwazuia kupewa makazi mapya au kuchelewesha kesi zao.
- Kutoweza kufikia nyenzo zilizo karibu au habari juu ya shughuli au haki ikiwa hawajashiriki hali yao na mashirika yasiyo ya kiserikali au mashirika ya kimataifa.⁵¹

“Duniani kote, wasagaji, wanawake wanaoshiriki ngono na jinsia zote, wabadili jinsia na wengine wenye mwelekeo tofauti wa kingono huwa wanaelekezewa dhuluma kali ya kimwili na kisakolojia. Huwa tunashambuliwa, kuvamiwa na kuelekezewa aina nyingine za dhuluma, mara nyingi ikisemekana ati ni kwa sababu ya ‘heshima, tamaduni, nchi na familia’.”

Nabulivou, N. (2013). *Statement on Behalf of the Lesbian, Bisexual and Transgender Caucus. Commission on the Status of Women, United Nations Economic and Social Council*

⁵¹ IOM/UNHCR, 2015, p. 16.

Wanawake na wasichana walio na ushirika tofauti wa kikabila na kidini

Wanawake na wasichana walio na ushirika tofauti wa kikabila na kidini mara nyingi hupuuza wakati wa kushughulikia dharura. Ikiwa dhuluma iliyosababisha ufurushwaji ililenga jumuiya maalum, wanawake na wasichana kutoka jumuiya hizo za kikabila au za kidini wanaweza kuwa katika hatari kubwa ya kuendelea kudhulumiwa na kubaguliwa. Baadhi ya makabila hayapati fursa za kiuchumi na yanakabiliwa na hatari kubwa zaidi ya biashara haramu ya binadamu, ikiwemo unyanyasaji wa kingono. Hatari hii huongezeka katika hali ambapo watu wamefurushwa makwao na inaathiri sana wanawake na wasichana walio na ushirika tofauti wa kikabila na kidini.⁵² Huenda wanawake na wasichana walio na ushirika tofauti wa kikabila na wa kidini wakatengwa zaidi na jamii na wanakosa ulinzi unaotoka kwa jumuiya ikilinganishwa na wale wa vikundi vinavyoongoza katika jamii. Wanawake na wasichana wenye ushirika tofauti wa kikabila na wa kidini wanaweza kupoteza vigezo muhimu vya utambulisho wao wa kitamaduni na sehemu ya utambulisho huu wa kitamaduni ufasiliwe visivyo au vibaya na mitandao ya kutoa usaidizi katika kipindi ambacho wametengwa wakati au baada ya kufurushwa. Jambo hili inaweza hasa kuwa hatari kwa wanawake na wasichana ambao wameathiriwa na unyanyasaji wa kijinsia. Wanawake na wasichana wanaweza kosa kuzungumza wazi ikiwa wakalimani wametoka jamii tofauti katika nchi ya asili au nchi walimokimbilia.⁵³

Kuna tofauti ndogo kati ya mahitaji ya kibinadamu ya vikundi na njia bora ya kukidhi mahitaji hayo, yaani hali, kulenga na kupeleka msaada. Tofauti hizo pia zinaonyesha ikiwa kikundi cha wachache kimelengwa moja kwa moja wakati wa mzozo, mateso na ubaguzi ambao wamewahi kupitia, kiwango chake cha nguvu za kisiasa au ushawishi na imani na kaida zake za kitamaduni.⁵⁴

Asasi nyingi za kibinadamu hazizingatii ushirika wa kikabila na kidini katika kuandaa mipango yao na umuhimu wa kabila na dini ya watu hupuuza kupitia njia inayotumiwa kukusanya habari.⁵⁵ Njia zinazotumiwa kushughulikia hali za kibinadamu zinahitaji kuzingatia utofauti huu ili kukidhi mahitaji muhimu ya wanawake na wasichana walioathiriwa na mizozo na kuwasaidia kwa njia endelevu. Lazima pia washughulikie vigezo vya jinsi wanavyoamua wanaopewa kipaumbele na kufaidika wakati wa kutoa msaada, mambo ambayo yanaweza kuendeleza chuki, ubaguzi na mvutano kwa kutenga baadhi ya vikundi vilivyoathiriwa na mizozo.⁵⁶

Asilimia 25 ya wanawake waliohojiwa katika tathmini ya haraka ya unyanyasaji wa kijinsia iliyofanywa kwa ajili ya uchunguzi wa kikanda wa 2016 ilionyesha kuwa ushirika wa kidini (na utaifa) uliathiri uwezo wao wa kupata huduma.⁵⁷ Huenda wanawake na wasichana kutoka vikundi tofauti vya kabila na dini wasijumuishwe katika vikao vya kusikiliza na kutathmini hivyo huenda mipango ya kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia isijumuishe mambo yenye kipaumbele kwao na mahitaji yao. Huenda habari ya jinsi ya kupata huduma zinazowalenga waathiriwa wa unyanyasaji wa kijinsia hazijatolewa kwa lugha tofauti. Huenda watoa huduma wanaoshughulikia waathiriwa wa unyanyasaji wa kijinsia hawazungumzi lugha zote za eneo husika au huenda wasiwahusishe watu wa kujitolea katika jamii na wakalimani ambao wanazungumza lugha tofauti. Huenda shughuli zinazofanywa katika nafasi salama za wanawake na wasichana hazipatikani kwa lugha tofauti. Wakati kabila au kikundi kimoja cha dini kinatawala shughuli za nafasi salama za wanawake na wasichana, vikundi vingine vya kikabila au kidini vinaweza kuhisi kama havifai kuwa pale. Baadhi ya shughuli za nafasi salama au za mipango ya kuwasaidia waathiriwa wa

⁵² UNHCR, Working With . . . , pgs. 10-11.

⁵³ UNHCR, Emergency Handbook, p. 3.

⁵⁴ Protection of Minorities in Iraq and Syria, p. 18.

⁵⁵ Protection of Minorities in Iraq and Syria, p. 14.

⁵⁶ Protection Needs of Minorities from Syria and Iraq, p. 3.

⁵⁷ Protection of Minorities in Iraq and Syria, p. 14.

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura
Mwongozo wa ujumuishaji

unyanyasaji wa kijinsia zinazojumuisha shughuli za kidini au za tamaduni za makabila au muziki, zinaweza kosa kuwajumuisha wanawake na wasichana wote anuwai.

Kiambatisho: Kuelewa "Ulemavu"

Kifungu cha 1 cha Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu (CRPD) kinafafanua watu wenye ulemavu kama ifuatavyo: "Watu wenye ulemavu ni pamoja na wale ambao wana udhaifu wa muda mrefu wa kimwili, kiakili, utambuzi au kuharibika kwa mifumo ya kufahamu ambao **kwa kuhusishwa na viziuzi vingine**, vinaweza kuzuia ushiriki kamili na madhubuti katika jamii kwa usawa na wengine" (msisitizo umeongezwa).⁵⁸

Wanawake na wasichana wenye ulemavu mara nyingi hufikiriwa kuwa wanahitaji msaada au kwa mtazamo wa kimatibabu, watu wanaohitaji matibabu, ukarabati na utunzaji. Mitazamo hii imeelezwa kama **mifano ya matibabu na msaada**. Mitazamo hii inayotokana na kuona ulemavu kama shida ya kibinafsi ambayo inapaswa kudhibitiwa, kutunzwa au kurekebishwa. Njia hii inaonyesha kwamba mwanamke anazuiwa kufanya kazi katika jamii na mwili au ubongo wake - na kwamba hili ni tatizo lake.

Mfano **unaojikita katika haki** unaona wanawake na wasichana wenye ulemavu kama wamiliki wa haki, hivyo kuhimiza nafasi kamili na sawa za kufurahia haki za binadamu kwa wanawake na wasichana wenye ulemavu, na heshima kwao kama binadamu. Njia hii inazingatia fursa sawa, kutobaguliwa kwa misingi ya ulemavu, na kushiriki katika jamii. Njia hii inayohimiza haki inahitaji mamlaka kuhakikisha haki zao wala si kuwazuia; kutekeleza sheria zinazohakikisha ujumuishaji kamili katika nyanja zote za kijamii (shule, familia, jamii, kazi n.k.); kutumia sera kuendeleza uhamasishaji; na kuheshimu kutambuliwa sawa mbele ya sheria.

Kanuni msingi ya jinsi haki za kibinadamu zinavyotazama ulemavu ni pamoja na kujumuisha, kushiriki, ufikiaji, kutobagua, kuheshimu tofauti na uanuwei, usawa wa nafasi na kuheshimu binadamu.

Mfano wa **kijamii ulibuniwa ili kupinga** mbinu za kibinafsi za mifano ya msaada na matibabu. Kulingana na mfano wa kijamii, ulemavu sio "kosa" la jamii lakini ni sehemu ya utofauti wake. Mfano wa kijamii unazingatia jamii na unachukulia kuwa tatizo liko katika jamii, kwamba wanawake na wasichana wenye ulemavu na Wanawake ambao ni wazee hutengwa kwa sababu ya viziuzi mbalimbali (mfano kijamii, kitaasisi, kiuchumi au kisiasa).⁵⁹ Yaani, kulingana na mfano wa kijamii⁶⁰ wa ulemavu, watu wenye ulemavu wanalemazwa na viziuzi vya kimfumo vinavyowakabili katika jamii, lakini si kwa sababu ya **toauti zao binafsi**. Kwa hivyo, inawezekana kuelewa neno "-enye ulemavu" kama "-liozuiwa kufanya kazi" badala ya "-enye uwezo mdogo."

Isitoshe, mfano wa kijamii hutofautisha kati ya "udhaifu" - vitu ambavyo mtu haziwezi kufanya kwa sababu ya mwili na / au ubongo wake - na "ulemavu", ambavyo ni **viziuzi vya kijamii vinavyomlemaza** mtu kwa sababu ana ugonjwa au udhaifu. Yaani, udhaifu ni sehemu moja tu ya ulemavu na inarejelea kazi ya mwili (kwa mfano, mtoto wa jicho anayezuia mwangaza kupita katika jicho, kupoteza mguu moja au kuathiriwa sehemu moja inayofanya kazi katika akili; vigezo vingine vya ulemavu ni viziuzi vya kuhusika na kushiriki katika shughuli, ambavyo ni sababu za mazingira.

Kuanza kufuata mfano wa kijamii kumehimiza ujumuishaji wa watu wenye ulemavu kwa kuondoa viziuzi na vikwazo badala ya kushughulikia udhaifu wa mtu binafsi kupitia mbinu maalum. Baadhi ya hatu ni pamoja na marekebisha ya ufikivu wa majengo, habari na mawasiliano ya ufikivu na kuhakikisha uwezo wa kupata huduma

⁵⁸ ADCAP Training, p. 22.

⁵⁹ ADCAP Training, p. 24.

⁶⁰ ADCAP Training, p.25.

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura
Mwongozo wa ujumuishaji

za msingi, utoaji wa vifaa vya kiufundi na vya kusaidia, kubadilisha mitizamo na kupunguza unyanyapaa, pamoja na kuwezesha watu wenye ulemavu na familia zao.

Ulemavu = Kudhoofika (kwa sehemu ya mwili wa mtu) + vizuizi (katika au kutoka kwenye mazingira)

'Ulemavu' si dosari ya asili kwa mwanamke au msichana; unatokana na mazingira kushindwa kukidhi mahitaji yake.

HATUA MUHIMU ZA KUBUNI MIPANGO SHIRIKISHI YA KUSHUGHULIKIA UNYANYASAJI WA KIJINSIA

Sehemu hii inazingatia hatua muhimu vya kubuni mipango jumuishi ya kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia; imeandaliwa kwa kutegemea muundo [wa Shirika la IRC wa Mpango wa Kujitayarisha na Kukabiliana na Unyanyasaji wa Kijinsia](#).

Tathmini⁶¹

Lazima tathmini ifanywe na uelewa kuwa **kila** jamii inajumuisha wasichana waliobalehe, wanawake ambao ni wazee, wanawake na wasichana wenye ulemavu, wanawake na wasichana walio na mitazamo tofauti ya kingono na utambulisho tofauti wa kijinsia na pia wanawake na wasichana kutoka ushirika tofauti wa kikabila na wa kidini. Hii ni pamoja na kuelewa kuwa wanawake na wasichana wanaweza kuwa na vitambulisho vingi vinavyopichasha. Si lazima ithibitishwe idadi ya wanawake na wasichana wenye ulemavu au uwepo wa wanawake na wasichana wenye mwelekeo tofauti wa kingono na utambulisho tofauti wa kijinsia ili mipango jumuishi na unayowasaidia wote ya kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia ibuniwe.

Kanuni Msingi ya 1 ya Sphere

Watu walioathiriwa ‘wanapaswa kuhusishwa kwa njia yenye maana katika maamuzi yanayoathiri maisha yao, bila kuongeza hatari zaidi. Hii ni njia moja ya kuwasaidia kutetea haki zao’.

Sphere Standards, YEAR, p. 1.

Kwa kuzingatia ukweli huu, lengo la tathmini yoyote linapaswa kuwa kushughulikia mahitaji anuwai ya wanawake na wasichana. Lengo la tathmini za unyanyasaji wa kijinsia si kutambua iwapo unyanyasaji huu unatokea. Lengo lake ni kuelewa vyema muktadha, mienendo ya dhuluma na huduma zilizopo za kuamua ni aina gani ya huduma na shughuli zinazofaa na zinazowezekana ili wanawake na wasichana wapone na wastawi. Isitoshe, uelewa thabiti wa hali za ukosefu wa usawa zinazowakabili wanawake na wasichana ni muhimu ili kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa - na shughuli za kupunguza hatari zinajumuishwa na zinapatikana kwa wanawake na wasichana wote - haziwaweki waathiriwa au watu wengine katika hatari zaidi. Hata hivyo, ni muhimu kutambua kwamba huenda baadhi ya wanawake na wasichana wakaogopa kutambuliwa waziwazi kama sehemu ya kikundi fulani cha utambulisho (mfano mshirika fulani wa kidini, kama mwanamke au msichana aliye na mwelekeo tofauti wa kingono na utambulisho tofauti wa kijinsia n.k.), kwa ujumla au miongoni mwa wanawake na wasichana walio katika idadi kubwa ya watu.

Inaweza kuwa muhimu kuhamasisha vikundi tofauti vya wanawake na wasichana kukidhi mahitaji ya lugha ya makabila anuwai ili kuhakikisha wasichana wa umri wowote wana uhuru wa kushiriki mambo wanayoyapatia kipaumbele, na kutoa nafasi kwa wanawake na wasichana wenye ulemavu kushiriki. Hata hivyo **HAIPENDEKEZWI kubuni vikundi tofauti kwa ajili ya wanawake na wasichana wenye mwelekeo tofauti wa kingono na utambulisho tofauti wa kijinsia** kwa sababu ya hatari za usalama na unyanyapaa unaojitokeza vikundi vinapobuniwa na kushirikishwa kwa misingi ya mwelekeo wa kingono na utambulisho wa kijinsia. Pia kuna faida za kubuni vikundi vilivyochanganyika vya wanawake tofauti na kuhimiza mazungumzo yanayohusisha tafsiri, lugha ya ishara, picha n.k. ili kuwezesha mazungumzo yanayowajumuisha wote waliopo na kuendeleza uelewa wa vipaumbele vya wote kati ya wanawake tofauti. Hata hivyo, **HAIPENDEKEZWI kuuliza wanawake na wasichana kufichua mwelekeo wao wa kingono au utambulisho wao wa kijinsia**. Wahudumu wanaoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia wanaweza kutumia njia ambayo tayari inatumika kujadili unyanyasaji wa kijinsia kwa kutumia hadithi zinazopishana za visa vilivyotokea na maswali ya jumla juu ya hatari ya unyanyasaji wa kijinsia ili

⁶¹ Session 3: Assessments – What Do We Need To Know To Start Programming and Session 4: Carrying Out Assessments, pages 27 - 40, GBV Emergency Preparedness & Response Participant Handbook <https://gbvresponders.org/emergency-response-preparedness/emergency-response-and-preparedness-training/>

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura
Mwongozo wa ujumuishaji

kujadili maswala nyeti na wanawake na wasichana kwa njia salama, bila kuwafanya wafichue visa binafsi vya dhuluma.

Mambo muhimu ya kujadili na wanawake na wasichana ni pamoja na kuuliza kuhusu:

- Wanawake na wasichana ambao wako katika hatari fulani ya kubaguliwa na kudhumiwa;
- Vizuizi maalum vinavyowakabili wanapojaribu kupata huduma;
- Mambo yanayoongeza hatari ya kunyanyaswa na kudhumiwa.
- Njia na mbinu ambazo zinaweza kusaidia vikundi maalum vya wanawake na wasichana kupata huduma na habari kwa njia salama.

Andaa tathmini ukizingatia maswali yafuatayo;

- Je, ni vikundi gani vya wanawake na wasichana ambavyo viko katika hatari kubwa zaidi kwenye jamii hii? Je, vikundi hivi vimetaja mahitaji, upungufu na vipaumbele gani?
- Je, ni vikundi gani vya wanawake na wasichana vinavyopata huduma? Je, ni vikundi gani ambavyo havipati huduma? Kwa nini? Tunawezaje kuwashirikisha zaidi?

Wakati wa kuandaa tathmini zingatia:

Wasichana waliobalehe: Kuwajumuisha wasichana waliobalehe, hasa wasichana wadogo (10 -14) katika mazoezi ya kukusanya habari kunaweza kuongeza hatari zaidi kuliko faida wakishiriki. Hatari zote zinapaswa kuzingatiwa kwa uangalifu kabla ya kushirikisha wasichana waliobalehe. Ikiwa juhudi za kupunguza hatari za kushiriki zimezidi faida za kushiriki, timu za kutathmini zinapaswa kuendelea na kuwashirikisha wanawake na wasichana hawa. Hata hivyo, ikiwa hatari zitaendelea kuzidi faida za kushiriki, ni lazima usalama wa wanawake na wasichana upewe kipaumbele juu ya kushiriki kwao katika shughuli za tathmini. Wasichana waliobalehe wana mahitaji na masilahi tofauti na ya wanawake wazima. Mara nyingi wao husema kuwa hawapendi kushiriki katika shughuli (zikiwemo za kukusanya habari) pamoja na mama zao. Huenda wasichana wanaoenda shuleni wana mahitaji na masilahi tofauti na ya wale wasioenda shuleni na wanapatikana kushiriki katika shughuli za tathmini katika nyakati tofauti.

Wanawake wenye umri wa juu mara nyingi huwa wana majukumu ya utunzaji wa watoto na familia, ambayo huwazuia kushiriki katika shughuli za tathmini. Sauti na vipaumbele vya wanawake wenye umri wa juu zaidi zinaweza kupuuzwa na viongozi wa jamii wanaohamasisha wanawake kushiriki katika tathmini. Wanawake ambao ni wazee wanaweza kuwa na matatizo ya kusafiri ikilinganishwa na wanawake wadogo au kutatizika kushiriki katika shughuli za kukusanya habari pamoja na wanawake wadogo kutokana na matatizo ya kusikia.

Wanawake na wasichana wenye ulemavu (wa kiwiliwili, kiakili, kifikra, kuona na kusikia) watahitaji njia mbalimbali za kuwasiliana na usaidizi katika kufikia na kushiriki katika majadiliano yanayohusiana na tathmini. Kwa mfano, nyongeza ya muda wa kujadili na kuuliza maswali, matumizi ya picha, wakalimani wa lugha ya ishara na mifano kwa kutumia maonyesho yanapaswa kuzingatiwa.⁶² Aidha, tathmini zinaweza kujumuisha mahojiano na wanaohudumia walemavu ili kuongoza muundo wa mpango wa kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia. Kama ilivyo kwa kikundi chochote cha jamii, huenda vikundi vya walemavu vinatawaliwa na wanaume. Jaribu kutambua

⁶² WGSS Assessment doc., p. 3-4.

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura
Mwongozo wa ujumuishaji

vikundi vya walemavu vinavyoongozwa na wanawake au uombe kuongea na wanawake wenye ulemavu ndani ya vikundi vya walemavu ili uelewe hatari na vizuizi mahususi vinavyowakabili wanawake katika jamii husika.

Wanawake na wasichana walio na mwelekeo tofauti wa kingono na utambulisho tofauti wa kijinsia hawapaswi kuwekwa katika vikundi tofauti katika jamii. Ili kuarifu tathmini yako kwa njia salama, hakikisha umewasiliana na wanaoshughulikia makundi ya LGBTQI, ambao wanaelewa mfumo wa kisheria na muktadha wa eneo husika. Hakikisha umezungumza na wanawake ndani ya jamii ya LGBTQI kwani jamii pia hii inaweza kuwa inatawaliwa na wanaume. Shirikisha vikundi vya LGBTQI vinavyoongozwa na wanawake mahali vinapatikana.

Wakati unazungumza na wanawake na wasichana wenye mwelekeo tofauti wa kingono na utambulisho tofauti wa kijinsia, kumbuka kuwataka kwa jina au kiwakilishi ambacho wamekwambia. Kama huna uhakika, uliza. Heshimu utambulisho wa wanawake na washichana. Hakikisha umethibitisha.

Wanawake na wasichana kutoka ushirika tofauti wa kikabila na kidini watahitaji maeneo na lugha tofauti ili kushiriki katika tathmini. Hakikisha kuwa hali ni salama vya kutosha kwa wanawake na wasichana kujisikia huru kujitambulisha kama washiriki wa kikundi fulani cha kikabila au kidini. Hii pia inahitaji kufahamu na kuamua kwa makini walio katika timu ya tathmini ili kuongeza kiwango cha uhuru wa wanawake na wasichana cha kushiriki. Hakikisha kuwa wanawake na wasichana ambao hawataki kujitambulisha hawalazimishi kufanya hivyo, hasa katika hali ambazo wanaweza kuwa katika hatari. Wakati wa kupanga mkutano na mtu au kikundi cha kabila au dini ya wachache, hakikisha kuwa hatua za kuhakikisha usalama na faragha yao zimechukuliwa.⁶³

Hatua muhimu:

- Shirikisha wanawake na wasichana kutoka vikundi tofauti kwa njia salama, usiamue vile wanavyofaa kushirikishwa bila ushahidi. Hakikisha kuwa umeuliza washiriki mapendeleo yao ili kuhakikisha kuwa wanawake na wasichana anuwai wako sawa na wanaweza kushiriki kwa njia salama.
- Katika majadiliano ya vikundi, tengeneza nafasi salama iwezekanavyo kwa kuimarisha usiri na kuwahakikishia washiriki kuwa si lazima washiriki maelezo ya kibinafsi ya visa vya unyanyasaji wa kijinsia au ubaguzi. Tutumia mifano ya kesi na ya jumla kujadiliana kuhusu jinsi vitambulisho tofauti vinaweza kuongeza hatari na vizuizi kwa wanawake na wasichana anuwai. Ikiwa mtu atazungumzia hali yake binafsi, ukumbushe kikundi kuhusu usiri.
- Usitambue wanawake na wasichana anuwai wanaoshiriki kwa kutaja au kubaini umri wa mwanamke, ulemavu, mwelekeo wa kingono, utambulisho wa kijinsia, dini, kabila au sifa nyingine, kwani kufanya hivi kunaweza kuwa na madhara na kusababisha unyanyapaa.
- Ikiwa wanawake na wasichana watajitambulisha na kushiriki mambo waliyoyapitia ambayo ni nyeti, basi kama ambavyo ungejibu kesi iliyoripotiwa ya unyanyasaji wa kijinsia, shukuru mshiriki kwa kusimulia aliyopitia, kumbusha kikundi kuhusu usiri na ueleze kwamba ikiwa Mshiriki angependa, basi uko tayari kuzungumza naye, kwa undani zaidi ana kwa ana, kuhusu yale aliyoyapitia baada ya majadiliano ya jumla ya kikundi. Hata hivyo, ikiwa mshiriki angependa kushiriki ndani ya kikundi, basi msaidie ili ashiriki na uheshimu chaguo lake la kuzungumza kuhusu aliyoyapitia ya kibaguzi na utambulisho wake. Kushiriki katika majadiliano ya nafasi salama inaweza kuwa nafasi ya kuwezesha wanawake tofauti na chaguo lao linafaa liheshimiwe.
- Tumia na ubadilishe zana za Tathmini za unyanyasaji wa kijinsia ambazo zinajumuisha wanawake na wasichana wote;
- Gawanya ukusanyaji wa data kwa misingi ya jinsia, umri, ulemavu na sifa zingine husika zinazoashiria ukosefu wa usawa;
- Nakili matokeo yanayofaa yanayoonyesha matukio waliyopitia wanawake na wasichana anuwai ili yazingatiwe katika kuandaa mpango wa kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia;

⁶³ UNHCR, Working With . . . , p. 7.

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura

Mwongozo wa ujumuishaji

- Wasiliana na watoa huduma ili utambue kaida na mitazamo inayoelezwa kwa wanawake na wasichana anuwai
- Hakikisha umetafsiri zana za tathmini ya unyanyasaji wa kijinsia kwa lugha tofauti zinazotumiwa na wanawake na wasichana kama iwezekanavyo;
- Husisha vikundi vinavyoshughulikia ujumuishaji kwenye eneo husika (mfano LGBTQI, wazee na wanaohudumia walemavu) katika upangaji wa tathmini, utoaji mafunzo kwa wafanyikazi na uhakiki wa zana.

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura
Mwongozo wa ujumuishaji

Jinsi Mpango Ulivyoandaliwa⁶⁴

Kuhakikisha kuwa wanawake na wasichana anuwai wanahusishwa katika uandaaji wa mpango mwanzoni mwa tukio la dharura na wakati wote wa kushughulikia tukio hilo kupitia njia za ufuatiliaji na ukusanyaji maoni ni hatua muhimu ya kutekeleza mpango jumishi wa kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia, jambo ambalo linaweza kushirikisha wanawake na wasichana anuwai kwa njia inayofaa. Kwa kutumia njia ya kuingiliana tangu mwanzo wa dharura kubuni mpango wa kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia, wanaoshughulikia unyanyasaji wa kijinsia wanaweza kushughulikia mizizi kali ya mapishano, ukandamizaji wa nguvu na fursa ambayo wanawake na wasichana kipekee wanapitia katika kupanga mipango ili kuhakikisha kuwa kikundi cha wanawake na wasichana anuwai kinaweza kushiriki na kufaidika na mpango huo⁶⁵. Kwa kuwashirikisha wanawake na wasichana anuwai katika majukumu ya uongozi katika kuandaa mpango wa kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura, wanaoshughulikia unyanyasaji wa kijinsia hutoa fursa kwa wanawake na wasichana anuwai kuwa mawakala na viongozi wanaoleta mabadiliko katika juhudi za ujenzi na ukarabati, zikiwemo kufanya uamuzi kuhusu maswala yanayoathiri usalama, ustawi na haki zao. Hii inaonekana kama njia bora zaidi ya kupingana na vyanzo msingi vya ubaguzi na kutengwa⁶⁶.

Hatua muhimu:

- Panga mipango ya kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia kwa pamoja na vikundi vya wanawake na wasichana anuwai tangu mwanzo wa dharura ili kuhakikisha kuwa mipango inayoshughulikia unyanyasaji wa kijinsia inarekebishwa ili kufaa muktadha wa eneo husika na inazingatia wanawake na wasichana;
- Gawanya data ya ufuatiliaji kwa misingi ya jinsia, umri wa walio walemavu, na vitambulisho vingine muhimu katika eneo husika;
- Hakikisha kuwa vikundi ambavyo vinahusishwa mara kwa mara katika mifumo ya uwajibikaji na utoaji maoni vina wawakilishi anuwai wa wanawake na wasichana;
- Hakikisha eneo la nafasi salama za dharura ni salama kwa wanawake na wasichana anuwai;
- Hakikisha shughuli za nafasi salama zimeundwa kwa njia ambayo zinaweza kupatikana kwa wanawake na wasichana anuwai;
- Zingatia mbinu mbalimbali za kuanzisha ujumuishaji wa wanawake na wasichana anuwai katika huduma za kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia. Shirikiana na watendaji wengine katika kuwawezesha kuzifikia huduma hizo, zikiwemo za afya, ulinzi kwa watoto, LGBTQI, ulemavu na wanaohudumia wazee;
- Buni timu za kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia katika eneo husika na uhakikishe zinajumuisha wati wanaozungumza lugha anuwai, wanawake wachanga na wazee, wanawake wenye ulemavu na wakati wa kutangaza nafasi za kazi, endeleza utofauti;
- Fundisha timu zinazoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia kutumia njia zinazolingiliana kutoka mwanzo wa dharura ili kuhakikisha timu zina mitazamo inayosaidia na zinaweza kutambua viashiria vya ukosefu wa usawa katika eneo husika.

⁶⁴ Session 5 Introducing the Program Model, page 41, GBV Emergency Preparedness & Response Participant Handbook
<https://gbvresponders.org/emergency-response-preparedness/emergency-response-and-preparedness-training/>
Christine Homan, Divya Chandran & Rita Lo (2018) Young feminists working

⁶⁵ [globally to end violence against women and girls: key challenges and ways forward](#), Gender & Development, 26:3, 495-513, DOI: 10.1080/13552074.2018.1525868

⁶⁶ HDN, p. 35. Humanitarian Exchange.

Kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia⁶⁷

Wanawake na wasichana anuwai wanahitaji kufikia huduma bora za usimamizi wa visa vya unyanyasaji wa kijinsia na utunzaji ulioratibiwa kwa njia salama na kwa wakati, unaofaa jinsia yao, umri, ulemavu, mwelekeo wao wa kingono, utambulisho wa kijinsia, kabila na dini. Usimamizi wa visa vya unyanyasaji wa kijinsia unaolenga mahitaji wa waathiriwa unatolewa ili kukidhi mahitaji ya kila mwathiriwa na kwa hivyo unaweza kukidhi mahitaji ya wanawake na wasichana anuwai kwa kuhakikisha ridhaa na usiri, kuheshimu matakwa yao na kutoa habari inayopatikana kuhusu huduma bila ubaguzi. Usimamizi wa visa vya unyanyasaji wa kijinsia unaolenga mahitaji wa waathiriwa umejengwa juu ya msingi kuwa mwathiriwa anaelewa hali yake mwenyewe zaidi ya vile anayemhudumia anavyoweza kuielewa. Kwa kutumia njia iliyozingatia waathiriwa, mwathiriwa ndiye anayefanya uamuzi na mfanyikazi anayeshughulikia kesi hiyo hutoa usaidizi bila vikwazo na uhusiano wa kusaidia mwathiriwa apone. Kwa hivyo, njia hii inafaa katika kusaidia waathiriwa wenye vitambulisho na hali tofauti wapone.

Katika hali za dharura, mara nyingi ni vigumu kutoa huduma kamili za kushughulikia kesi mbalimbali. Mahitaji na chaguzi msingi za waathiriwa zinapaswa kupewa kipaumbele, zikiwemo ulinzi na usalama, ufikiaji wa huduma za afya na usaidizi wa kisaikolojia.⁶⁸ Ni lazima huduma zinazosimamia na kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia ziwe jumuiishi na zishughulikie mahitaji ya wanawake na wasichana anuwai. Watoa huduma wanaoshughulikia unyanyasaji wa kijinsia wana jukumu la kitaalam la kuhudumia kwa usawa kila mwanawake na msichana kwa heshima. Wakati wa kutoa mafunzo kwa wafanyikazi wanaoshughulikia kesi ya unyanyasaji wa kijinsia, ni muhimu kutoa fursa kwa timu husika kutambua na kuchunguza ubaguzi ulio ndani ili kuhakikisha wanawahudumia waathiriwa kwa njia isiyo na ubaguzi na kwa huruma, bila kuwahukumu.

Hatua muhimu:

- Kagua na utambue huduma ili ubaini huduma zilizopo za kushughulikia kesi hizi na upungufu kwa kuzingatia mahitaji anuwai ya wanawake na wasichana na ubuni mpango wa kushughulikia upatikanaji muhimu wa huduma au upungufu katika uwezo kwa ushirikiano na wadau na mashirika muhimu yanayoshughulikia unyanyasaji wa kijinsia.
- Hakikisha kuna njia mbalimbali za kuanza kupata huduma kando na zile zinazosimamia visa vya unyanyasaji wa kijinsia na uunganishe wanawake na wasichana na huduma za usaidizi wa kisaikolojia.
- Tafuta na uajiri wafanyikazi / wanaojitolea wanaowakilisha uanuwai uliopo katika jamii wa wanawake na wasichana.
- Wasaidie watoa huduma wanaoshughulikia unyanyasaji wa kijinsia kwa kuwapa mafunzo ya usimamizi wa kesi yanayozingatia waathiriwa ambayo yanalenga na ni mahsusi kwa wasichana waliobalehe, wanawake ambao ni wazee, wanawake na wasichana wenye ulemavu, wanawake na wasichana walio na mitazamo tofauti ya kingono, utambulisho tofauti wa kijinsia, ushirika wa kabila na dini tofauti.
- Fuatilia upatikanaji wa huduma na ubora wa utunzaji ambao unakidhi mahitaji anuwai ya wanawake na wasichana waathiriwa wa unyanyasaji wa kijinsia kupitia tafiti zinazokusanya maoni ya wateja kwa siri, usimamizi unaoendelea wa waoshughulikia kesi na majadiliano kupitia vikao vya mara kwa mara vya kutoa maoni na vikundi na wanawake na wasichana anuwai.
- Imarisha ujumuishaji wa wanawake na wasichana anuwai katika njia ya uelekezaji kwa kushirikisha wahudumu wenye ulemavu, wazee na walio wa kikundi cha LGBTQI na viongozi kutoka makabila na dini tofauti katika njia hii ya uelekezaji.
- Toa mafunzo ya kuhamasisha ujumuishaji na uanuwai kwa wafanyikazi, wahudumu wanaoshughulikia kesi na watoa huduma wanaoshughulikia unyanyasaji wa kijinsia;

⁶⁷ Session 6 Case Management, page 46-49, GBV Emergency Preparedness & Response Participant Handbook <https://gbvresponders.org/emergency-response-preparedness/emergency-response-and-preparedness-training/>

⁶⁸ UNFPA MS, p. 56.

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura
Mwongozo wa ujumuishaji

- Tumia matukio, mbinu bora, usaidizi na huduma kutoka kwa watendaji katika eneo husika wanaofanya kazi na wanawake na wasichana anuwai yaani, wanaowahudumia wenye ulemavu, wazee na wana-LGBTQI.

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura
Mwongozo wa ujumuishaji

Kiambatisho cha jinsi ya Kushughulikia kesi ya Unyanyasaji wa Kijinsia: Mambo ya kuzingatia wakati wa kuhudumia na kusaidia waathirika wenye ulemavu:

Mawasiliano

Mara nyingi, waathiriwa wenye ulemavu wanaweza kuwasiliana moja kwa moja na wasaidizi au watoa huduma bila marekebisho yoyote, au marekebisho machache, kama vile kutambua mtu anayeweza kutafsiri aina ya lugha ya ishara wanayoitumau kwa kutumia lugha rahisi katika majadiliano. Katika hali zingine, huenda njia bora ya kuwasiliana na mwathiriwa ikawa si bayana, na ikahitaji hatua za ziada ili kuitambua njia mwafaka. Wakati unafanya kazi na wanawake na wasichana wenye ulemavu ambao wanaona ugumu kuwasiliana, unapaswa:

Kuchukua wakati, kuangalia na kusikiliza. Ikiwa uko katika muktadha ambapo utaweza kuona mwathiriwa zaidi ya mara moja, kumbuka kwamba kushughulikia kesi ni mchakato, sio tukio la wakati mmoja. Kila wakati unapokutana na mwathiriwa, utajifunza jambo jipya juu yake na kuelewa vizuri jinsi anavyowasiliana na anachomaanisha.

Zungumza moja kwa moja na mwathiriwa, hata kama mlezi wake yupo. Ikiwa bado unajaribu kutambua njia za kuwasiliana na mwathiriwa na unahitaji kuomba ushauri kutoka kwa mlezi wake, hakikisha kuwa mazungumzo haya yanafanyika mbele ya mwathiriwa, ili asikie kinachosemwa na ashiriki kwa njia yoyote inayoweza. Kumbuka kwamba wanawake na wasichana ambao hawawezi kuongea au kusonga bado wanaweza kuelewa kinaendelea karibu nao na kile watu wanasema juu yao.

Tilia makini njia yoyote ambayo wanawake na wasichana wanapenda kutumia kuwasiliana. Baadhi ya njia hizi ni kama kupitia ishara na wakati mwingine hisia zao. Baadhi ya wanawake na wasichana wenye ulemavu wa kiakili na kisaikolojia wanaweza kuonyesha tabia mbalimbali. Hii ndiyo njia ambayo wakati mwingine wao hutumia kuwasiliana na wengine. Ikiona au uhisi kwamba mwathiriwa anajaribu kuwasiliana nawe lakini huelewi, ni sawa kusema "Sielewi."

Usimshinikize mwathiriwa. Mara nyingi kiwango cha kuelewa au kufanya kazi cha waathiriwa wenye ulemavu wa kiakili na kukua hurudi nyuma wakati wameshinikwa. Daima heshimu utayari wa mtu mwenyewe kuzungumza juu ya matukio. Kama ilivyo kwa mwathiriwa yeyote, jihadhari na kuiga mienendo ya kutumia nguvu na udhibiti bila kujua kwa kushinikiza mwathiriwa atoe habari ambazo bado hayuko tayari kuzizungumzia.⁶⁹

Utoaji Idhini na Ufanyaji Maamuzi⁷⁰

Mkataba ya Haki za Watu wenye Ulemavu unaangazia kwamba watu wenye ulemavu wana haki sawa na kila mtu mwingine kufanya maamuzi yao, na kwamba lazima hatua zinazofaa zichukuliwe ili kuwasaidia kutumia uwezo wao wa kisheria. Mtu hawezi kupoteza uwezo wake wa kisheria wa kufanya maamuzi kwa sababu ana ulemavu. Mwanzo, unapaswa kuchukulia kuwa waathiriwa wote ambao ni watu wazima wenye ulemavu wana uwezo wa kutoa idhini wao wenyewe. Wakati wote, muulize mtu huyo kama angependa kupata usaidizi ili afanye uamuzi wenye maarifa.

Ikiwa unafanya kazi na mtu ambaye unapata shida kuwasiliana naye, jiulize maswali muhimu yafuatayo:

- Je, umejaribu zaidi ya njia moja ya kuwasilisha habari hiyo? Je, umewapatia muda wa kuchakata habari hii na kuuliza maswali?
- Una njia ya kutambua ikiwa mwathiriwa anaelewa habari inayotolewa na matokeo ya maamuzi ambayo atafanya?Ulifikiaje uamuzi huu? (mfano: kupitia maswali, majadiliano, ishara au aina nyingine?)
- Umeweza kuhakikisha kuwa maamuzi ya mwathiriwa ni ya hiari wala si ya kushinikizwa au kulazimishwa na wengine?Ulifikiaje uamuzi huu?

⁶⁹ Interagency GBV Case Management Guidelines, p. 139. <https://gbvresponders.org/response/gbv-case-management/>, p. 143.

⁷⁰ Interagency GBV Case Management Guidelines, p. 139. <https://gbvresponders.org/response/gbv-case-management/>, p. 143.

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura
Mwongozo wa ujumuishaji

- (Je, kuna mlezi au mwanafamilia ambaye tayari amehusishwa? ikiwa kunaye, amehusishwa vipi? Je, anajibu maswali unayouliza kwa ushauriano na mwathiriwa?)

Ikiwa baada ya kutafakari maswali haya bado huna uhakika wa uwezo wa mwathiriwa kutoa idhini yeye mwenyewe, unapaswa kuhusisha msimamizi ili akusaidie kuamua ikiwa kuna haja ya kutoa usaidizi zaidi ili mpate idhini. Wewe na msimamizi wako mnaweza kujadiliana juu ya kuchukua hatua zifuatazo:

Fikiria kumshirikisha mtu wa kuaminika anayeweza kusaidia. Wanafamilia, walezi na marafiki wa watu wenye ulemavu wanaweza kuwa rasilimali muhimu katika kuwezesha uelewa na mawasiliano na mtu huyo. Mkiona ni hatua salama ya kuchukua, ombeni ruhusa ya mwathiriwa ya kumjumuisha mtu anayemwamini katika mazungumzo yenu kama njia ya kuwezesha mawasiliano na kuboresha uwezo wa mwathiriwa kutoa idhini. Acha mwathiriwa atambue mtu ambaye angependa kumshirikisha na mwangalie ishara zozote kwamba anakubali au hakubaliani na maoni yanayotolewa na anayesaidia. Mnahitaji kuangalia kwa makini kwamba mtu anayetoa usaidizi si yeye anayefanya uamuzi.

Tathmini ni yapi yanayomfaa zaidi mwathiriwa. Mwishowe, ikiwa bado huna uhakika wa uwezo wa mwathiriwa wa kutoa idhini wakati wowote katika mchakato wa usimamizi wa kesi, basi unaweza kutumia kanuni zifuatazo za kufikia uamuzi unaomfaa zaidi mwathiriwa.

Usalama: Je, uamuzi au hatua hiyo inamlinda mwathiriwa kutokana na dhuluma inayoweza kumpata (ya kimwili, kihemko, kisaikolojia na kingono n.k.)?

Uwezeshaji: Je, uamuzi au hatua hiyo inaambatana na tafsiri bora ya matakwa na matakwa ya mwathirika?

Uchambuzi wa faida na gharama: Je, faida inayoweza kutokana na uamuzi au hatua hiyo inazidi hatari zinazoweza kutokea?

Uponyaji: Je, uamuzi au hatua hiyo inaendeleza upataji nafuu, ukuaji, na kupona kwa mwathiriwa?

Kwa kiwango kinachowezezekana, bado unapaswa kupata idhini kutoka kwa mwathiriwa (yaani aseme ako tayari kushiriki katika maamuzi, huduma na / au shughuli zinazopendekezwa).

Kufanya kazi na Walezi au Wanafamilia

Kama ilivyojadiliwa katika sehemu zilizopita, kufanya kazi na walezi au wanafamilia linaweza kuwa jambo linalosaidia sana na katika hali zingine, jambo la lazima. Hata hivyo, kufanya hivyo pia kunaweza kutatiza juhudi za kuendeleza usalama, usiri na masilahi ya mwathiriwa. Watu wenye ulemavu wanapaswa kushauriwa kila wakati juu ya ushirikishaji wa walezi na wanafamilia, kama ilivyo na waathiriwa wote. Utahitaji kutathimini mara kwa mara hatari na faida za kuhusisha mlezi wa mwathiriwa na uulize kila wakati ikiwa ni jambo la lazima, salama na ambalo mwishowe linamwezesha mwathiriwa. Mambo muhimu kukumbuka wakati unafanya kazi na walezi na wanafamilia ni:

Tathmini usalama. Mara kwa mara fanya tathmini kamili ya usalama ili uhakikishe mtu anayesaidia hamnyanyasi mwathiriwa kwani mara nyingi, anayenyanyasa huwa ni mtu ambaye mwathiriwa anajua na anaweza kuwa mtu anayemtunza na kumsaidia kila siku.

Zingatia mwathiriwa. Mwathiriwa ndiye anayehitaji kuhudumiwa na vitendo vyote vinapaswa kuongozwa na ridhaa na mapendeleo yake. Huenda masilahi ya wanafamilia na walezi yawe au hasiwe yanahusiana na ridhaa na mapendeleo ya mwathiriwa. Msingi, shirikisha na uwasiliane na mwathiriwa na umwombe yeye ruhusa ya kuwasiliana na mwanafamilia au mlezi wake.

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura
Mwongozo wa ujumuishaji

Dumisha usiri. Ikiwa mwathiriwa atashiriki habari ambazo hataki mlezi wake au wanafamilia wajue, lazima uheshimu uamuzi wake na udumishe usiri. Usishiriki habari zozote za mwathiriwa, hata na mlezi wake, bila ruhusa ya wazi kutoka kwa mwathiriwa. Wakati wa kushiriki habari, jiulize kila wakati sababu za mlezi kutaka habari hiyo na ushiriki tu yale anayohitaji ili kuwezesha utunzaji Kwa mfano, unaweza kufanya kikao cha pamoja na mwathiriwa na mlezi wake ili kukagua mpango wa hatua wa kesi yake kwa sababu kuna mahali ambapo mlezi au mwanafamilia anahitajika kuchangia. Katika hali hiyo, wanahitaji tu kujua kinachofaa ili kuwezesha sehemu hiyo ya utunzaji wa mwathiriwa. Mwishowe, ikiwa mlezi au mwanafamilia anahusika katika sehemu yoyote ya mchakato wa usimamizi wa kesi, anahitaji pia kudumisha usiri. Hakikisha tangu mwanzo umemwelezea mtu huyo suala hili wazi.

Msaidie mlezi au mwanafamilia. Ukishathibitisha kuwa mlezi au mwanafamilia ni salama, unapaswa kumsaidia pia. Kuwapatia habari sahihi juu ya hatari na athari za unyanyasaji wa kijinsia na kiwewe kunaweza kuwasaidia kuelewa anayopitia mwathiriwa na njia bora zaidi ya kumsaidia. Walezi wanaweza kumlaumu mwathiriwa, kwa hivyo hakikisha umewaeleza kuwa kilichotokea hakikuwa kosa la mwathiriwa. Walezi wanaweza pia kujilaumu kwa kutoweza kumlinda mwathiriwa kutokana na dhuluma. Kuwapa walezi ujumbe wa kuwatia moyo, usiwalaumu wala kuwahukumu linaweza kuwa jambo muhimu kwao kusikia. Kwa kuwasaidia, unaongeza pia uwezo wao wa kusaidia mwathiriwa.⁷¹ Walezi wa wasichana wenye ulemavu wanaweza pia kuwa wanatatizika kukubali au kukabiliana na ulemavu huo. Huenda wakawa wanafikiria kuwalazimisha au kuwaingiza katika ndoa za mapema na mwanaume au mvulana ili wajiondolee mzigo wa kumlea. Wafanyikazi wanaoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia wanapaswa kufahamu kuwa wasichana wenye ulemavu wanaweza kuwa katika hatari kubwa ya ndoa ya kulazimishwa au ya mapema katika hali zingine na watafute njia za kupunguza hatari hizi kwa pamoja na mwathiriwa kupitia mchakato wa usimamizi wa kesi.

Usalama

Mipango ya usalama kwa waathiriwa walemavu lazima imlenge mtu binafsi na inapaswa kuzingatia yafuatayo:

- Ulemavu mahususi na hali ya maisha ya mwathiriwa na njia ambazo yule anayeendeleza unyanyasaji huu anaweza kujaribu kutumia ulemavu wa mwathiriwa ili kumtenga, kumzuia asiondoke au kumdhuru zaidi.
- Jinsi ulemavu wa mwathiriwa unavyoweza kuathiri utekelezaji wa mpango wake wa usalama, na urekebishe mpango kama inahitajika.
- Vitu mahususi kwa ulemavu ambavyo mtu huyo atahitaji ikiwa atatumia mpango wake wa usalama, kama vile dawa, zana au vifaa vya kusaidia au nyaraka zinazofaa kwa msaada wa afya au kisheria.⁷²

⁷¹ IAGBVCML, p. 146.

⁷² IAGBVCML, p. 146.

Msaada wa Kisaikolojia⁷³

Unga mkono utoaji wa huduma za kisaikolojia zinazozingatia utamaduni, umri na jinsia ili kuhakikisha kwamba walioathiriwa na matukio ya kiwewe wanapata ulinzi na ukarabati wa kutosha ili waweze kujumuika tena katika jamii. Hakikisha kuwa njia zinazofaa na zinazofanya kazi vilivyo za urejelezi zinapatikana kwa wanawake na wasichana. Kubagua na kutowajumuisha wanawake na wasichana kutoka vikundi mbalimbali katika usaidizi na huduma za kisaikolojia zinazoshughukilia visa vya unyanyasaji huongeza idadi ya waathiriwa, athari hasi za kisaikolojia na matatizo ya kiafya.

Njia za kuelezea dhiki - jinsi wanawake na wasichana wanavyoelezea na kuelewa dalili zao za kiafya na jinsi wanavyotafuta usaidizi - ni maalum kwa tamaduni, na zimejikita katika dini na kaida za kijamii. Kwa hivyo asili ya wanawake na wasichana ya dini na kabila ni muhimu katika kuelewa na kukidhi mahitaji ya waathiriwa wa unyanyasaji wa kijinsia. Kwa mfano, wanahitaji kuwa na imani na watoa huduma ili wajitokeze, na katika hali zingine, wanawake hujihisi huru kupokea msaada kutoka kwa wafanyikazi walio katika imani sawa. Kutambua familia na utamaduni wa jamii waliyotoka wanawake ni muhimu katika kusaidia waathiriwa wa unyanyasaji wa kijinsia kwani maswala yanayozunguka faragha, tabia za nyumbani na mila wakati mwingine hutofautiana na kutoyazingatia kunaweza kuwazuia wanawake kupata usaidizi wanaohitaji.⁷⁴ Tumia miundo ya asasi za kiraia zilizopo zinazoaminika na wakazi wa eneo hilo, zikiwemo zile za makundi tofauti ya kikabila na kidini ili kutoa habari juu ya huduma za kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia.

Mbinu bora: kujumuisha tena katika jamii wanawake wa Yezidi waliokuwa watumwa

Shirika la Yazda, linaloshirikiana na NCA, kwa ushirikiano na viongozi wa kidini wa Yezidi kule Lalish (mahali patakatifu pa Yezidi nje ya Dohuk) limebuni utaratibu wa kujumuisha tena katika jamii wanawake waliokuwa wametekwa nyara na IS. Mwanzoni mwa utaratibu huu, wanawake hawa hutembelea eneo la Lalish kwa siku chache, wanapokea ushauri nasaha na kufanyiwa matambiko ya kutakaswa, kabla mapadri huko Larish wawakubalie, mbele ya umma, kujiunga tena na jamii ya Yezidi. Mapadri hawa pia hutangaza hadharani kuwa wanawake hawa hawakuchangia katika yale yaliyowatendelea na wanafaa kukubaliwa wajiunge na familia na jamii zao bila chuki wala ubaguzi wowote.

Protection of Minorities in Iraq and

Hatua muhimu:

- Kufunza na kutoa usaidizi kwa wanaofika kwanza wakati wa visa vya unyanyasaji wa kijinsia ili watoe mazingira salama na tulivu; wasikilize kwa makini; waonyeshe huruma na wasihukumu; watoe uhakikisho bila upendeleo na wawezeshe upatikanaji wa huduma kwa wanawake na wasichana anuwai;
- Kutoa msaada wa kisaikolojia unaoambatana na umri, ulemavu, utamaduni na dini ya wanawake na wasichana anuwai;
- Kuhakikisha habari juu ya huduma za usaidizi wa kisaikolojia zinashirikiwa na kufikia wanawake na wasichana anuwai kwa kuwalengwa wao hasa;
- Kutambua na kuondoa viziwi vinavyowazuia wanawake na wasichana anuwa kupata huduma za msaada wa kisaikolojia vikiwemo: eneo, uwezo wa kusafiri na ufikiaji, gharama, faragha, lugha, sababu za kitamaduni (mfano haja ya ruhusa au kuandamana na jamaa wa kiume), utunzaji wa watoto, muda wa shughuli n.k.⁷⁵
- Kutambua na kukuza kikundi cha kusaaidiana kilichojikita katika jamii, mikakati ya kujisaidia na kuimarisha uvumilivu, ikiwemo kufanya kazi na jamii, watoa huduma na wanaharakati katika eneo husika ili kuanzisha au kurekebisha taratibu na desturi ambazo zinaweza kuwezesha msaada wa jamii ambao unakuza ujumuishaji, usalama, heshima, utunzaji na kupona;
- Kuongeza huduma jumuiishi za Mifumo ya Bidhaa na Huduma (PSS) katika njia ya uelekezaji, kuhakikisha uelekezaji salama, unaodumisha siri kwa huduma za utunzaji wa afyaya jumla na ya akili au huduma za kliniki

⁷³ Session 7 Psychosocial Support, page 50 -58, GBV Emergency Preparedness & Response Participant Handbook <https://gbvresponders.org/emergency-response-preparedness/emergency-response-and-preparedness-training/>

⁷⁴ Protection of Minorities in Syria and Iraq, p. 13.

⁷⁵ IASC MHPSS Protection, p. 9-10.

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura
Mwongozo wa ujumuishaji

na huduma zingine za ulinzi, shughuli zinazokuza na kuwezesha uchumaji kipato kwa wanawake na wasichana anuwai.

Nafasi salama za Wanawake na Wasichana (WGSS)

Nafasi salama ya wanawake na wasichana ni mahali ambapo wanawake na wasichana katika utofauti wao wote wanaheshimiwa na kukaribishwa. Wafanyikazi na wahudumu wa kujitolea wanapaswa kufahamu na kushauriana na wanawake na wasichana kuhusu jinsi ya kurekebisha miundo na shughuli za burudani katika nafasi hizi salama ili kuwajumuisha wanawake na wasichana wa kila umri, walemavu, wenye mwelekeo tofauti wa kingono, utambulisho tofauti wa kijinsia, kabila na dini tofauti. Wanawake na wasichana anuwai wanapaswa kujihisi salama kisaikolojia na kimihemko kwenda kwenye nafasi salama ili kuripoti matatizo ya ulinzi, kuelezea mahitaji yao, kupokea huduma, kushiriki katika shughuli za uwezesaji na uchumaji kipato, kusaidia na kuunganika na wanawake na wasichana wengine. Nafasi hizi salama zinapaswa kutoa nafasi kwa watetezi, wawakilishi na uongozi wa wanawake na wasichana anuwai na kuchukua hatua ili kuongeza ushiriki wao wenye maana katika huduma na shughuli zinazoendelea katika nafasi hizo.

Nafasi zilizotengewa wanawake na wasichana anuwai mara nyingi huwa hazikidhi mahitaji yao maalum. Nafasi yoyote salama inapaswa kulenga kuwa na shughuli mbalimbali ambazo zinaweza kukidhi mahitaji anuwai ya wanawake na wasichana na kujenga vuguvugu la wanawake anuwai, kuwaunganisha wanawake na wasichana waliohamishwa katika jamii mpya. Kwa ujumla, watoa huduma wanaoshughulikia unyanyasaji wa kijinsia wanafaa kulenga kurekebisha shughuli za nafasi salama ili ziweze kupatikana kwa urahisi, badala ya kupanga shughuli maalum kwa vikundi vilivyotengwa. Wakati huna uhakika, wasiliana na wanawake na wasichana anuwai na ujenge uelewa wa pamoja wa mahitaji anuwai. Ikiwa kutakuwa na mzozo au ushindani kati ya wanawake na wasichana anuwai, panga vipindi vya kusikiliza na majadiliano ili kuwezesha washiriki walio katika nafasi hizi salama waweze kuhisi maono ya kila mmoja na waelewe hali ambayo kila mmoja amepitia. Kwa mfano, maadhimisho ya hafla za kidini yanaweza kuwa nafasi muhimu ya kuleta jamii za dini mbalimbali pamoja na kukuza stahamala ya dini zingine. Inapendekezwa kuwa na nafasi tofauti za wasichana waliobalehe katika nafasi hizi salama ili kutoa nafasi yenye shughuli maalum zinazofaa umri. Hata hivyo, kushiriki mambo uliyojifunza katika nafasi salama za wasichana hawa na jamii pana ya wanawake na wasichana huendeleza uelewa na usaidizi wa jamii kwa mahitaji ya wasichana waliobalehe. Vivyo hivyo, kusherehekea au kuandaa hafla za uhamasishaji katika siku za kimataifa zinazoangazia masuala ya ulemavu, uzee, au haki za LGBTQ, kunaweza kujenga ufahamu na kukuza stahamala katika jamii pana ya wanawake na wasichana.

Hatua muhimu;

- Kushirikisha kimaksudi wanawake na wasichana anuwai katika kuunda nafasi salama za wanawake na wasichana;
- Kupanga kamati ya nafasi salama za wanawake na wasichana ili kuendesha shughuli za nafasi hizo salama ambazi ni pamoja na uwakilishi wa wanawake na wasichana anuwai;
- Kuajiri wafanyakazi na wahudumu wa kujitolea wa kuendesha shughuli za nafasi hizo salama ambao wanawakilisha wanawake na wasichana anuwai katika jamii;
- Kutumia idadi inayofaa ya lugha zinazozungumzwa katika jamii na njia mbadala za mawasiliano ili kufikia wanawake na wasichana anuwai katika jamii;
- Kutoa mafunzo ya kuhamasisha ujumuishaji na utofauti kwa wafanyikazi na wahudumu wa kujitolea katika nafasi hizi salama, kuwashirikisha katika shughuli endelevu ya kutafakari na kujitambua ili kuona upendeleo wanaoweza kuwa nao, uwezo wa kimalaka na fursa ambazo zinathiri wanawake na wasichana anuwai;
- Kushirikisha wanawake na wasichana kikamilifu kupitia mikakati ya kuwafikia ili kupunguza vizuizi vya upatikanaji ambavyo vinawazuia wanawake na wasichana anuwai kushiriki kwa njia inayofaa;

Mahali salama na ambapo wanawake na wasichana wenye mwelekeo tofauti wa kingono na utambulisho tofauti wa kijinsia wanahisi wamekaribishwa Kuendeleza na kusherekea uanuwai katika nafasi salama. Kuheshimu na kukubali wanawake na wasichana jinsi walivyo. Kuuliza wanawake na wasichana jinsia wangependa kushiriki katika shughuli za nafasi salama. Kukuza matumizi ya istilahi

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura
Mwongozo wa ujumuishaji

- Kugawanya maoni ya wanaoshiriki katika nafasi hizi salama kuhusu kuandaa mipango kwa misingi ya umri, ulemavu na ukosefu mwingine wa usawa katika eneo hilo na kushughulikia mapengo na vizuizi vya kushiriki.

Huduma za Afya⁷⁶

Ufikiaji wa huduma bora za afya, kwa usiri, zinazofaa umri na zinazotolewa kwa njia inayofaa binadamu ni sehemu muhimu na inayookoa maisha ya huduma zinazotolewa na sekta mbalimbali za kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia katika miktadha ya dharura. Wahudumu wa afya mara nyingi huwa ndio wa kwanza na wakati mwingine wahudumu pekee ambao waathiriwa wa unyanyasaji wa kijinsia huwasiliana nao. Wanawake na washichana anuwai wanaweza kuwafikia kwa njia salama kwa sababu za kiafya bila kubainisha kuwa wanahitaji matibabu ya unyanyasaji wa kijinsia hadi wawe katika mahali faragha. Wahudumu wa afya wako katika mstari wa mbele wa kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura na wanachukua jukumu kuu katika kutambua masuala ya ulinzi yanayoathiri wanawake na wasichana anuwai, kushughulikia mara moja mahitaji ya kiakili na kihemko / kisaikolojia, na kutoa nafasi ya kufikia huduma zinazopatikana za kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia na nafasi salama zilizotengewa wanawake na wasichana waathiriwa.⁷⁷ Wahudumu wa afya wanaelewa jukumu lao la kutoa huduma za kitaalam ambazo ni za siri, bila kumhukumu wala kumbagua yeyote. Hata hivyo kama ilivyo na wahudumu wote wanaoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia, wahudumu wa afya wanaweza kunufaika na fursa za kutambua na kuchunguza upendeleo wao wa ndani na mitazamo hasi ili kuhakikisha wanatoa huduma kwa njia adilifu, bila ubaguzi.

Hatua muhimu:

- Kuhakikisha wanawake na wasichana anuwai wanafikia mara moja huduma za afya ya uzazi kama ilivyoainishwa kwenye Kifurushi cha Huduma Msingi ya Kwanza (MISP) mwanzoni mwa dharura (hakuna haja ya kutathmini mahitaji);⁷⁸
- Kuhakikisha wanawake na wasichana wote anuwai walioathiriwa na unyanyasaji wa kijinsia wanapata huduma za afya za ubora wa juu, zinazoweza kuokoa maisha, zikiwemo matibabu ya ubakaji katika kituo cha afya na yale ya baadaye yanayotolewa kwa wakati unaofaa;
- Kushauriana na wanawake na wasichana anuwai katika kubuni na kutoa mipango ya huduma za unyanyasaji wa kijinsia na za afya.
- Kuendeleza vikundi vya msaada vya wanawake, ikiwemo kutoa mafunzo ya au msaada maalum wa kujumuisha vikundi tofauti katika jamii kulingana na umri wao, ulemavu na vitambulisho vingine.
- Kwa kutumia mifumo ya uratibu wa afya, kuwezesha zoezi la utambuzi / uchambuzi wa Huduma za Afya ya Ngono na Uzazi (SRH) zikiwemo vikundi maalum vya mitaa au watoa huduma ambao tayari wanafanya kazi na wanawake na wasichana anuwai, kutambua mahitaji, uwezo na mapungufu ya mpango wa Huduma za Afya ya Ngono na Uzazi na kuandaa zoezi la kupanga kwa kushirikiana na wadau wote husika ili kuwezesha utoaji wa huduma bora na zinazofaa za afya na kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya haudhoofishwi na mitazamo ya wafanyikazi, mienendo ya nguvu kulingana na vipengele vya ukosefu wa usawa vinavyopishana vinavyowakabili wanawake na wasichana anuwai.
- Kujumuisha kikamilifu shughuli ya kufikishia jamii huduma ambayo inaongozwa na jamii yenyewe; mfanyikazi wa afya katika jamii, wakunga wanaotumia mbinu za jadi, wanaopigia debe masuala ya usafi, wafanyakazi katika vikundi vya wanawake na wale wanaofikisha huduma kwa jamii ili kujumuisha kikamilifu wanawake na wasichana anuwai katika kutafuta suluhu za athari za unyanyasaji wa kijinsia zinazogusa huduma zinazotolewa za afya ya jumla na ya ngono na uzazi.

Kutagusana na waathiriwa wenye ulemavu kunahusu watu, wala si ulemavu.

IRC.

⁷⁶ Session 8 Health Response, page 59 - 70, GBV Emergency Preparedness & Response Participant Handbook <https://gbvresponders.org/emergency-response-preparedness/emergency-response-and-preparedness-training/>

⁷⁷ UNFPA MS, p. 24.

⁷⁸ The Sphere Project, Sexual and Reproductive Health Standard 1, <http://www.spherehandbook.org/en/essential-healthservices-sexual-and-reproductive-health-standard-1-reproductive-health/>

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura

Mwongozo wa ujumuishaji

- Kutambua, kukusanya na kuchambua mfumo wa maelezo ya afya uliogawanywa kwa misingi ya jinsia, umri, ulemavu na vitambulisho vingine ili kufuatilia shughuli za kupunguza hatari za unyanyasaji wa kijinsia, ufikiaji na vizuizi kwa huduma za afya.
- Lazima wafanyikazi wa afya wapewe mafunzo ya jinsi ya kutoa huduma zinazoambatana na umri na zinazowafaa walemavu. Ni lazima ujenzo wa uwezo wa wahudumu katika vituo vya afya ujumuishe aina anuwai ya watu, uwe hauna ubaguzi, upunguze unyanyapaa, mienendo ya nguvu na haki za kupata huduma.
- Kushirikiana na wahudumu katika eneo husika, wataalamu wa jinsia, wataalam wa utofauti, mitandao inayoshughulikia ujumuishaji kama vile vikundi vya wazee, ulemavu, LGBTQI, kabila au dini katika utoaji wa huduma za afya.

Mifumo ya Uelekezaji⁷⁹

Waathiriwa wa unyanyasaji wa kijinsia wana mahitaji mengi, na uratibu kati ya watoa huduma ni muhimu katika kusaidia wanawake na wasichana kukidhi mahitaji hayo. Mifumo ya uelekezaji maaluma kwa muktadha husika huratibu utoaji wa huduma na kuwezesha waathiriwa kufikia huduma. Katika miktadha ya dharura, waathiriwa wa unyanyasaji wa kijinsia kutoka asili tofauti wanahitaji kufikia huduma za kuokoa maisha haraka na kwa njia salama. Kwa kiwango cha chini, wanawake na wasichana anuwai wanahitaji (1) mtandao wa watoa huduma waliohitimu; na (2) njia rasmi ya uelekezaji inayoelezea ni wapi na ni jinsi gani waathiriwa wanaweza kupata huduma.⁸⁰

Njia ya uelekezaji ni mbinu rahisi ambayo inaunganisha kwa njia salama wanawake na wasichana waathiriwa wa unyanyasaji wa kijinsia kwa huduma za usaidizi na katika muktadha wa dharura, njia za uelekezaji hutoa kipaumbele kwa ufikiaji salama wa huduma ya afya na ya kisaikolojia. Mfumo mzuri wa uelekezaji unampatia mwathiriwa kipaumbele na unajumuisha wanawake na wasichana anuwai ambao ni waathiriwa. Wanawake na wasichana anuwai wanaweza kupata habari kuhusu huduma zinazoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia wakati wanashiriki katika harakati zingine za mabadiliko ya kijamii. Kuandaa wahudumu katika miktadha ya kibinadamu wanaoshughulikia masuala ya walemavu, wazee, wana-LGBTQI kwa kuwapa uelewa wa njia ya uelekezaji katika kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia, kuwatasaidia kuelekeza wanawake na wasichana ambao wanafichua kuwa wanapitia unyanyasaji wa kijinsia mahali wanapoweza kupata usaidizi. Kuhusisha vikundi hivi kunaweza pia kusaidia wanaoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia kujua juu ya huduma tofauti zilizopo za kukidhi mahitaji ya wanawake na wasichana anuwai.

Hatua muhimu:

- Wakati wa shughuli ya [kutambua huduma zilizopo za unyanyasaji wa kijinsia](#), jumuisha vigezo vinavyopima uwezo jumuishi wa wanawake na wasichana anuwai kufikia huduma;
- Shirikisha wadau wanaotetea mabadiliko na ujumuishaji katika jamii kama vile vikundi vinavyoshughulikia masuala ya ulemavu, LGBTQI, wazee, haki za watoto na vijana ili kuhakikisha wanafahamu njia ya uelekezaji katika kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia na kusaidia wanawake na wasichana kutoka vikundi hivi kupata huduma;
- Hakikisha njia za uelekezaji zinapatikana kwa wanawake na wasichana anuwai kupitia mbinu anuwai: redio za lugha nyingi, mabango yaliyo na maandishi ya nukta nundu, lugha ya ishara kwenye hafla za jamii, n.k.;
- Zingatia kwa uangalifu jinsi wasichana waliobalehe wanaweza kufikia huduma zinazoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia kupitia mipango inayoshughulikia visa hivi na ile ya ulinzi wa watoto;
- Fuatilia maoni kutoka kwa wanawake na wasichana anuwai yanayoangazia vizuizi na ufikiaji katika mfumo wa uelekezaji na uchukue hatua za kuondoa vizuizi na kuongeza ufikiaji kwa wanawake na wasichana anuwai ili waweze kufikia huduma za sekta mbalimbali;
- Patia watoa huduma wajibu wa kuzingatia mahitaji anuwai na ujumuishaji wa wanawake na wasichana anuwai kupitia uratibu iliopo na taratibu msingi za utekelezaji (SoPs).

⁷⁹ Session 9 Referral Systems, page 71 - 77, GBV Emergency Preparedness & Response Participant Handbook <https://gbvresponders.org/emergency-response-preparedness/emergency-response-and-preparedness-training/>

⁸⁰ UNFPA MS, p. 54.

Kufikisha huduma kwa jamii⁸¹

Katika muktadha wa dharura, hatua ya kufikisha huduma kwa jamii huwezesha wanaoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia kushiriki habari na wanajamii ili kusaidia wanawake na wasichana anuwai kupata huduma za kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia na kupunguza hatari zinazowakabili wanawake na wasichana hawa. Kufikisha huduma kwa jamii kunajumuisha habari juu ya faida za huduma zinazoshughulikia visa vya nyanyasaji wa kijinsia, namna, mahali na wakati wa kuzipata huduma hizi, ambazo zinapaswa kupatikana kwa wanawake na wasichana anuwai. Kufikisha huduma kwa jamii kunatoa fursa ya kuonyesha mipango jumuishi ya kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia kupitia picha, lugha na vifaa vinavyotumika kukuza uelewa na ufikiaji wa huduma zinazoshughulikia unyanyasaji huu. Kushirikisha wanawake anuwai kama wafanyikazi na wahudumu wa kujitolea wa jamii kunaweza kuonyesha mfano mwema wa ujumuishaji na kufanya huduma zivutie na zipatikane zaidi kwa wanawake na wasichana anuwai katika jamii. Mabango, vipindi vya redio na kampeni zinazolenga umma kwa jumla zinaweza kuwakilisha wanawake na wasichana anuwai kwa njia chanya, kukuza kutambuliwa kwa haki na hadhi sawa na kuonyesha wanawake na wasichana anuwai wanaounga mkono na kufanya kazi kwa pamoja kuzuia unyanyasaji wa kijinsia.

Hatua muhimu:

- Hakikisha timu za wanaoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia zinazopeleka huduma kwa jamii zina washiriki anuwai iwezekanavyo na zinajumuisha wafanyikazi na wahudumu wa kujitolea kutoka vikundi anuwai vya wanawake ukizingatia umri, vikundi vya lugha na ulemavu;
- Hakikisha nyenzo za maelezo, mafunzo na mawasiliano zinazoshiriki habari ya kueneza huduma zinazoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia na kuhimiza watu kuzungumza kuhusu visa vya unyanyasaji huu zinajumuisha wawakilishi kutoka jumuiya anuwai na zinaweza kufikiwa na vikundi vyote vya lugha;
- Tumia redio na nyenzo za maelezo, mafunzo na mawasiliano zenye michoro ili kufikia wanawake na wasichana wenye ulemavu wa kuona na kusikia;
- Tumia njia mbalimbali za kufikia jamii zinazotimiza mahitaji ya wanawake na wasichana anuwai, kwa mfano, kuwafikia wasichana waliobalehe ndani na nje ya shule, kupanga nyakati na sehemu tofauti za kukutana ili kushirikisha wanawake na wasichana anuwai zaidi, n.k.;
- Shirikiana na wahudumu wengine wanaotetea ujumuishaji na mabadiliko ya kijamii kama vile wale wanaofanya kazi na wazee, wenye ulemavu na wana-LGBTQI pamoja na viongozi wa jamii na wa kidini kutoka makabila na dini tofauti ili kuandaa hafla za kufikisha huduma kwa jamii ambazo zinalinga vikundi maalum vya wanawake na wasichana anuwai na jamii pana;
- Jadiliana na wasichana waliobalehe na walezi wao wa kike na wa kiume kuhusu jinsi ya kushirikisha wasichana hawa katika kuongoza aina fulani ya shughuli za kufikia wanarika zao katika jamii kwa njia salama;
- Fuata mwongozo wa nyenzo za mawasiliano kwa kuonyesha wanawake na wasichana anuwai kwa njia nzuri, kwa mfano kama wanawasaidia wengine au kama watetezi;
- Andaa vikao vya kusikiliza na wanawake na wasichana anuwai au njia zingine wanazopendelea za kutoa maoni juu ya shughuli za kufikia jamii na kurekebisha mipango kulingana na mapendekezo ya wanawake na wasichana anuwai.

⁸¹ Session 10 Community Outreach, page 78 - 80, GBV Emergency Preparedness & Response Participant Handbook <https://gbvresponders.org/emergency-response-preparedness/emergency-response-and-preparedness-training/>

Kupunguza Hatari kwa Wanawake na Wasichana katika Hali za Dharura⁸²

Katika hali za dharura, wanawake na wasichana anuwai wanakabiliwa na hatari nyingi za usalama zinazohusishwa na kufurushwa. Nyingi za hatari hizi zinapogundulika, zinaweza kushughulikiwa kwa haraka na kwa njia salama na wahudumu wa kibinadamu. Hata hivyo, mashirika ya misaada ya kibinadamu yanaweza kuongeza hatari hizi bila kukusudia kupitia mipango na huduma za kutoa msaada zilizoundwa ili kuboresha utendaji bora bila kutambua vizuri na kushughulikia mahitaji ya wanawake na wasichana anuwai na vizuizi ambavyo huenda vikawakabili katika kufikia huduma kwa njia salama.

Wahudumu wanaoshughulikia unyanyasaji wa kijinsia wanapotekeleza mipango jumuishiya ambayo inashirikisha na kusaidia wanawake na wasichana anuwai kwa njia inayofaa, basi shughuli za kupunguza hatari za unyanyasaji wa kijinsia zitaonyesha hatari na vizuizi maalum vinavyowakabili wanawake na wasichana anuwai katika kila muktadha. Pia kuna shughuli nyingi za kupunguza hatari za unyanyasaji wa kijinsia zinazoweza kufanywa kila mara ili kukidhi mahitaji ya wanawake na wasichana anuwai katika kila muktadha. Kwa mfano katika kila muktadha wa kibinadamu, vyoo na sehemu za kuogea zinapaswa kutengwa kulingana na jinsia, umri unaofaa, ziwe zimefungwa, zina mwangaza wa kutosha, ziko mahali ambapo wanawake na wasichana wanaweza kuzifikia kwa usalama na mahali ambapo wanawake na wasichana wenye ulemavu na walio na matatizo ya kutembea wanaweza kufika bila kutatizika. Isitoshe, maji na fueli zinapaswa kuwa mahali ambapo wanawake na wasichana wanaweza kufikia kwa usalama. Wanawake ambao ni wazee, wanawake na wasichana wenye ulemavu, wanawake walio na watoto wachanga, wanawake wajawazito na wasichana waliobalehe wanapaswa pia kuweza kuzifikia. Wanawake na wasichana anuwai wanafaa kuweza kufikia makaazi, chakula, sehemu za kusambazia pesa na NFI, programu za masomo na za uchumaji kipato. Zote hizi zinafaa kuambatana na mahitaji yao. Ufuatiliaji unapaswa kufanywa ili kuhakikisha wanawake na wasichana anuwai wanaweza kufikia mahitaji haya msingi kwa usawa na kwa njia salama.

Hatua za kupunguza hatari ya unyanyasaji wa kijinsia zinapaswa kujumuisha kupunguza hatari ya ukatili na unyanyasaji wa kingono (SEA) unaoendelezwa na wahudumu wa kibinadamu. kuna uwezekano wa wanawake na wasichana ambao wanakabiliwa na ukosefu wa usawa kutokana na umri, ulemavu, mwelekeo wa kingono, utambulisho wa kijinsia, kabila, dini na viini vingine vya ukandamizaji, kulengwa na kudhulumiwa na wahudumu wa kibinadamu. Hatua ya kuwajumuisha na kumakinikia vizuizi na hatari zinazowakabili katika upataji wa misaada ya kibinadamu ni kipaumbele katika mpango wa kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia.

Hatua muhimu:

- Chukulia kuwa unyanyasaji wa kijinsia unaathiri wanawake na wasichana anuwai katika kila muktadha na kutekeleza hatua jumuishi za kupunguza hatari ya unyanyasaji wa kijinsia, ikiwemo kupunguza hatari ya ukatili na unyanyasaji wa kingono;
- Washawishi wahudumu wa kibinadamu kushughulikia hatari na vizuizi vilivyotambuliwa vinavyoathiri wanawake na wasichana anuwai kupitia uratibu na utetezi;
- Kagua hatua za kupunguza hatari zilizo katika mwongozo wa unyanyasaji wa kijinsia ili kuzizingatia katika uchambuzi wako wa usalama na kuzingatia vizuizi na hatari tofauti zinazowakabili wanawake na wasichana anuwai kwa kila huduma ya kibinadamu;
- Tumia [ukaguzi wa usalama](#) uliorekebishwa ambao unajumuisha maswali ambayo yanaonyesha hatari na vizuizi maalum vinavyowakabili wanawake na wasichana anuwai;
- Zungumza mara kwa mara na wanawake na wasichana juu ya hatari za unyanyasaji wa kijinsia zinazowakabili wanawake na wasichana anuwai na mikakati ya kuzishughulikia;

⁸² Session 11 Reducing Risks for Women & Girls in Emergencies, page 81 - 88, GBV Emergency Preparedness & Response Participant Handbook
<https://gbvresponders.org/emergency-response-preparedness/emergency-response-and-preparedness-training/>

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura

Mwongozo wa ujumuishaji

- Tambua mikakati, kwa kushauriana na wanawake na wasichana anuwai, ili kuondoa vikwazo vinavyowazuia kushiriki na kupata misaada inayotolewa, ufikiaji wa huduma, kushiriki katika shughuli (kwa mfano muda, eneo, usalama wa kusafiri, usalama wa shughuli);
- Endeleza ushiriki wenye maana wa wanawake na wasichana anuwai katika upangaji na maamuzi ya mipango ya kibinadamu.

Kudhibiti na Kushiriki Habari⁸³

Ni muhimu kuzingatia jinsi tunavyotumia na sababu tulizo nazo za kutumia habari kuhusu wanawake na wasichana anuwai waathiriwa wa unyanyasaji wa kijinsia katika muktadha wa dharura na kufuata kanuni thabiti za maadili katika ukusanyaji wa data. Ukusanyaji wa data ya unyanyasaji wa kijinsia ni suala nyeti sana, hasa katika muktadha wa utoaji wa huduma. Usimamizi wa data hiyo si rahisi na unahitaji kuwe na mifumo na mbinu za ulinzi ili kuhakikisha usalama wa data na usalama wa kila mtu anayehusika kwa sababu kukusanya na kushiriki habari hii kunaweza kuwa hatari kwa waathiriwa wanaopiga ripoti, jamii na hata wale wanaohusika katika kukusanya habari hiyo.⁸⁴ Kukusanya data ya unyanyasaji wa kijinsia kunajumuisha hata kuilinda.⁸⁵ Kuheshimu itifaki za kushiriki habari kati ya mashirika na mashirika yote husika ni sehemu muhimu ya usalama wa wanawake na wasichana walioathiriwa, hasa wale walio hatarini.

Fomu za kutoa ridhaa pamoja na zile za kurekodi visa vya unyanyasaji wa kijinsia kawaida hurekodi⁸⁶ maelezo ya umri, ulemavu na kabila. Kwa hivyo, wanaoshughulika na visa hizi huweza, kama sehemu ya uchambuzi wa data ya huduma za kawaida, kutathmini ikiwa wasichana waliobalehe, wanawake ambao ni wazee, wanawake na wasichana wenye ulemavu na kutoka kabila tofauti, wanafikia huduma zinazoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia. Katika mahali ambapo hawapati huduma, mahojiano ya moja kwa moja au majadiliano ya vikundi yanapendekezwa ili kubaini vizuizi vya upatikanaji wa huduma. Mahali ambapo kuna data ya idadi ya watu inayojumuisha maelezo ya umri, ulemavu na kabila la wanawake na wasichana, inawezekana kuchambua ikiwa visa vya unyanyasaji wa kijinsia vinavyoripotiwa vinaambatana na idadi ya watu katika eneo hilo.

Pia, mahali popote ambapo pana wanawake na wasichana waliofurushwa makwao, patakuwa na wanawake na wasichana wenye mwelekeo tofauti wa kingono na utambulisho tofauti wa kijinsia. Baada ya kufunza timu yako inayoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia ili kuhakikisha wanajumuisha wanawake na wasichana anuwai na ambapo ni salama kufanya hivyo, unaweza kuongeza sehemu iliyo kando ya kujadili masuala ya mwelekeo wa kingono na utambulisho wa kijinsia. Kwa mfano, unaweza kuwa na sehemu inayouliza: Wanaojitambua kwa kinsia waliyozaliwa nayo au mwanamke aliyebadili jinsia kama sehemu ya utambulisho wa kijinsia; na wasagaji, wanaoshiriki ngono na watu wa jinsia zote mbili au wanaoshiriki na jinsia moja ili kubainisha mwelekeo wa kingono. Usibadilishe fomu ya kurekodi kisa ili kuongeza sehemu juu ya mwelekeo wa kingono na utambulisho wa kijinsia bila kutoa mafunzo kwa wafanyikazi wako kwanza na kuhakikisha huduma zinajumuisha wanawake na wasichana anuwai. Katika maeneo ambapo kuwa msagaji, kushiriki ngono na jinsia zote mbili au kubadili jinsia ni hatia - usirekodi mwelekeo wao wa kingono.

2-Survivor Information		
Date of birth (approximate if necessary)*:	Sex*: ☐ Female ☐ Male	Clan or ethnicity:
Country of origin* ⁸⁴ :	☐ Country names here ☐ Etc.	☐ Other (specify) : ☐ Etc.
Nationality (If different than country of origin):		Religion:
Current civil / marital status*:	☐ Single ☐ Married / Cohabiting	☐ Divorced / Separated ☐ Widowed

⁸³ Session 13 Information Management and Sharing, pages 89- 94, GBV Emergency Preparedness & Response Participant Handbook <https://gbvresponders.org/emergency-response-preparedness/emergency-response-and-preparedness-training/>

⁸⁴ GBVIMS, User Guide, p. 2.3.

⁸⁵ GBVIMS Facilitators' Guide, p. 21.

⁸⁶ <http://www.gbvims.com/gbvims-tools/intake-form/>

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura
Mwongozo wa ujumuishaji

[Fomu ya GBVIMS hukusanya](#) maelezo ya umri, ulemavu na kabila

Hatua muhimu:

- Chukulia kuwa unyanyasaji wa kijinsia inafanyika kwa wanawake na wasichana anuwai katika kila muktadha na utekeleze mipango ya kushughulikia unyanyasaji huu - usingoje kukusanya data kwanza!
- Hakikisha fomu za ridhaa zinafaa kutumiwa na wanawake na wasichana anuwai, yakiwemo lugha, umri, uwezo, na uwezo wa ukuaji wa mteja;
- Tumia fomu za kawaida za kurekodi kisa cha unyanyasaji wa kijinsia kurekodi habari kuhusu utofauti wa wanawake na wasichana kwa njia salama na uzihifadhi kwa usiri katika kabati lililofungwa au hifadhidata iliyosimbwa;
- Tumia data iliyokusanywa katika fomu ya kurekodi kisa cha unyanyasaji wa kijinsia kukamilisha uchambuzi wa taratibu na kubuni mapendekezo ya mipango kulingana na upatikanaji wa huduma kwa vikundi tofauti vya wanawake na wasichana;
- Hakikisha wahudumu wote wanaoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia wakitumia fomu ya kurekodi kisa cha unyanyasaji yenye vidokezo vya ziada vya data kwa wanawake na wasichana wenye mwelekeo tofauti wa kingono na tambulisho tofauti wa kijinsia wanapata mafunzo kwanza kuhusu mipango jumuishi ya kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia;
- Hakikisha data ya wanawake na wasichana waathiriwa wa unyanyasaji wa kijinsia imehifadhiwa kwa njia salama na inatumika kwa kuzingatia maadili ili kuboresha utayarishaji wa mipango na kutoa huduma bora.

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura
Mwongozo wa ujumuishaji

Uratibu na Utetezi⁸⁷

Uratibu na utetezi vinaungana kwa karibu na zinalenga kuhakikisha rasilimali, msaada na mipango inatumika vizuri kwa ajili ya wanawake na wasichana anuwai. Utetezi ni pingele cha kawaida katika kazi ya kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia na ni muhimu kwa kila kiwango cha kuingilia kati - muundo, mfumo na utekelezaji - wakati wa kushughulikia ukatili dhidi ya wanawake na wasichana katika mikatdha ya dharura.

Kutumia data na masimulizi juu ya wanawake na wasichana kwa ajili ya utetezi wakati wa dharura kunahitaji kuzingatia kwa makini mwongozo wa maadili uliowekwa kulinda wanawake na wasichana na kupunguza hatari za mipango ya unyanyasaji wa kijinsia katika mikatdha ya dharura. Wakati wa kugawanya data ili kuonyesha mahitaji maalum ya wanawake na wasichana anuwai, ni muhimu bado kuhakikisha kuwa data hii haitambulishi wahusika na ni salama kushiriki. Inawezekana kuwa kubainisha sana utambulisho wa mwanamke au msichana kutamweka katika hatari ya kushambuliwa na aliyeendeleza uhalifu huo ili kulipiza kisasi, kubaguliwa au madhara kutoka kwa jamii.

Ili kukamilisha uchambuzi wa kuangalia shida katika mkakati jumuishi wa utetezi, zingatia kuongeza maswali yafuatayo ya kutafakari:

- Je, ni shida gani zinawakabili wanawake na wasichana katika jamii?
- Kipaumbele muhimu zaidi kwa wanawake ni kipi? Je, kipaumbele hiki ni sawa na cha wanawake na wasichana anuwai?
- Kwa nini hili ni tatizo?
- Ni nini kinafaa kufanywa ili kutatua tatizo hili na kusaidia wanawake au waathiriwa? Je, suluhisho hili pia linawafaa wanawake na wasichana anuwai?
- Ni suluhisho lipi lenye uwezekano zaidi wa kufanikiwa? Je, kuna wanawake na wasichana wowote tunaowatenga?
- Je, tunawezaje kuhakikisha kuwa njia ambayo mahitaji ya wanawake na wasichana anuwai yanaangaziwa kupitia utetezi haihatarishi usalama wao?
- Je, tunawezaje kuhakikisha kuwa yaliyomo katika ujumbe wetu wa utetezi juu ya mahitaji ya wanawake na wasichana anuwai hayahatarishi usalama wao?
- Je, kuna athari zozote zisizotarajiwa za mawasiliano ya utetezi au uratibu zinazoweza kuwadhuru wanawake na wasichana? Je, hatari hizi zinaweza kupunguzwa?

Kuongana kwa vuguvugu za mabadiliko ya kijamii kunaweza kuwa njia nzuri ya kuongeza ufanisi wa utetezi unaoshughulikia unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya wanawake na wasichana anuwai katika mikatdha ya dharura na kunatoa fursa kwa vuguvugu zingine za mabadiliko ya kijamii kuzingatia unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya wanawake na wasichana anuwai na kuangazia suala hili katika utetezi wao juu ya ulemavu, uzee, LGBTQI au haki za watoto.

Hatua muhimu:

- Hakikisha kampeni na hafla za utetezi zinashirikisha wanaharakati wanawake na wasichana mbalimbali kwa njia salama na kwa kuzingatia maadili;
- Unga mkono uwakilishi wa wanawake na wasichana anuwai katika muundo wa uongozi wa jamii na kuendeleza ukuzaji wa uwezo wa viongozi wa kike katika masuala ya haki za wanawake, ujuzi wa uongozi, ustadi wa kujadili na kuzungumza mbele ya umma⁸⁸;
- Wakati wa kushawishi viongozi wa kibinadamu na wafadhili kupitia shughuli za utetezi, hakikisha hadithi na sauti za wanawake na wasichana anuwai zinawakilishwa;

⁸⁷ Session 14 Coordination and Advocacy in Emergencies, page 96-104, GBV Emergency Preparedness & Response Participant Handbook <https://gbvresponders.org/emergency-response-preparedness/emergency-response-and-preparedness-training/>

⁸⁸ GBV Minimum Standard for Women's Participation and Empowerment (*forthcoming*)

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura
Mwongozo wa ujumuishaji

- Hakikisha uchambuzi wa tatizo katika mkakati wa utetezi unaonyesha hatari na vizuizi vinavyoathiri wanawake na wasichana anuwai na unatoa suluhisho kutoka kwa wanawake na wasichana anuwai;
- Katika ripoti au hafla za utetezi za kieneo, kitaifa au kimataifa, tumia data na hadithi kwa njia salama na inayozingatia maadili kuonyesha mahitaji na vipaumbele vya wanawake na wasichana anuwai;
- Wakati wa kutambua na kufanya kazi na washirika katika ngazi ya eneo na ya kimataifa, shirikiana na vuguvugu mbalimbali ili kushirikisha zile zinazoshughulikia ulemavu, LGBTQI, uzee, haki za watoto na harakati zingine za mabadiliko ya kijamii.

Kuwa Tayarisha na Mipango ya Kukabiliana na Dharura⁸⁹

Mipango wa kujitayarisha ili kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura unakusudia kuanzisha uwezo wa kushughulikia visa vya dhuluma dhidi ya wanawake na wasichana katika hali tofauti za mizozo ya kibinadamu ambazo zinaweza kuathiri nchi au ukanda kwa kuweka seti pana ya hatua za utayari. Kuweka vifaa mapema ni shughuli muhimu ya kujiandaa kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia. Fikiria kama wakati wa kuandaa vifaa vya kuhifadhi hadhi, taratibu za usafi zinazozingatiwa ni tofauti kwa makabila anuwai ambayo yanaweza kuwa yameathiriwa na mzozo katika muktadha wa eneo hilo. Wakati wa kuunda nyenzo za maelezo, mafunzo na mawasiliano zenye ujumbe rahisi wa kukuza ufikiaji wa huduma katika muktadha wa dharura, hakikisha lugha inajumuisha makabila anuwai na picha za wanawake na wasichana zinajumuisha wanawake na wasichana wa umri na makabila tofauti, wenye ulemavu na aina mbalimbali za utambulisho wa kijinsia.

Kufundisha vikundi tofauti vya wanawake na wahudumu wanaoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia kutoka eneo husika, kuwa tayari kushughulikia hali ya dharura ni shughuli nyingine muhimu ya kujiandaa kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia ambayo inatoa fursa ya kutekeleza mipango jumuishi ya kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia. Hakikisha unashirikisha vikundi vya wanawake katika vuguvugu kubwa za mabadiliko ya kijamii. Kwa mfano, nenda kwa mashirika ya watu wenye ulemavu au vikundi vya haki za LGBTQI au jamii za kidini na makabila ili kujua ikiwa wana vikundi vya wanawake; uliza ikiwa vikundi au vikao vya vijana vina vikundi vya wasichana waliobalehe na kadhalika.

Mashirika mengi yanaweza kupanga shughuli zao za kujitayarisha kwa kutoa mafunzo kwa timu inayoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia inayoweza kuitwa kukiwa na tukio la dharura. Ni muhimu kuhakikisha timu yako inayoshughulikia visa hivi vya unyanyasaji wa kijinsia inajumuisha watu anuwai. Hakikisha kuwa wanawake waliopewa wajibu wa kusimamia timu na kutoa huduma wametoka katika mazingira anuwai.

Hatua muhimu:

- Kagua orodha ya vifaa au zana za dharura na uhakikishe kuwa vifaa vimehifadhiwa na vinapatikana kwa wanawake na wasichana anuwai, vikiwemo vifaa vya hadhi na vifaa vya maelezo, mafunzo na mawasiliano;
- Wakati wa kufunza vikundi vya wanawake na mashirika yanayoongozwa na wanawake kwenye mazingira yaliyo katika hatari ya mzozo, huhakikisha mmetambua na kutoa mafunzo kwa vikundi ambavyo vinasaidia na vinajumuisha wanawake na wasichana anuwai;
- Wakati wa kutekeleza mafunzo ya kujitayarisha kwa wahudumu wanaoshughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia katika eneo husika, wafanyikazi wa jamii na wafanyikazi wa afya kwenye mazingira yaliyo katika hatari ya mzozo, kusudia kuwashirikisha watoa huduma wa kike kutoka ulingo mpana wa makabila na lugha, umri, wanawake wenye ulemavu, na watoa huduma wanaoshughulikia masuala ya kijinsia;
- Wakati wa kutekeleza shughuli za kujitayarisha kwa kutambua huduma za kujitayarisha, hakikisha umekagua njia ya uelekezaji ili uhakikishe inapatiakana na uongeze katika vidokezo vya ziada vya kuingia ili kukidhi mahitaji ya wanawake na wasichana anuwai katika muktadha wa eneo husika;
- Hakikisha njia ya uelekezaji imeshirikiwa na vikundi vinavyohusika na mabadiliko ya kijamii na mashirika ambayo yanafanya kazi na wanawake na wasichana anuwai katika eneo husika;
- Angalia bajeti yenu ya kujitayarisha ili kuhakikisha rasilimali zimetengwa ili kutoa mipango jumuishi ya kushughulikia visa vya unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake na wasichana wote;
- Sasisha na ujumuishe masuala ya hatari, usalama na ulinzi wa wafanyikazi kutoka mazingira tofauti. Hakikisha hatua za kurekebisha zimechukuliwa ili kuhakikisha utoaji jumuishi wa huduma kwa wanawake na wasichana wakati matatizo yanatambuliwa. ;

⁸⁹ Session 15 Emergency Preparedness, page 106-110, GBV Emergency Preparedness & Response Participant Handbook
<https://gbvresponders.org/emergency-response-preparedness/emergency-response-and-preparedness-training/>

Zana ya kujitayarisha ili kushughulikia unyanyasaji wa kijinsia wakati wa dharura
Mwongozo wa ujumuishaji

- Jumuisha uhamasishaji juu ya utofauti na ujumuishaji katika mafunzo kwa wafanyakazi ya kujitayarisha na kushughulikia visa vya dharura vya unyanyasaji wa kijinsia.